HOJAJI

YA

TATHMINI

YA

APRM

1. HISTORIA YA MCHAKATO WA APRM

1. 1. Utangulizi

1. 1. 1. Waraka wa Msingi wa APPRM [AHG/235(XXXVIII) Annex 2] unafasili APRM kama Mkataba ambao umekubaliwa na Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kama mchakato wa kujifanyia tathmini.

1. 1. 2. Lengo la msingi la APRM ni "kuhimiza utumiaji wa sera, viwango na matendo ambayo yanajenga utengamano wa kisiasa, ukuaji kasi wa uchumi, maendeleo endelevu na kuharakisha ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda na bara zima kwa ujumla kwa kubadilishana uzoefu na kuimarisha mafanikio na matendo mema ikiwa ni pamoja na kutambua upungufu na kutathmini mahitaji kwa ajili ya kujijengea uwezo.

1. 1. 3. Ili kuhakikisha kwamba lengo la msingi linafikiwa, nchi washiriki zimeahidi kutumia sheria, sera na viwango, ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa watu na asasi. Zimeahidi pia kutumia malengo, viwango na viashiria maalum kutathmini na kufuatilia kwa karibu maendeleo katika maeneo muhimu kwa kuongozwa na waraka wa msingi wa APRM. na Azimio la NEPAD kuhusu utawala katika Demokrasia, Siasa, Uchumi na Makampuni kama ilivyotangazwa na Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika (AU) uliofanyika Durban, Afrika Kusini mwezi Julai, 2002 [AHG/235 XXXVIII Annex 1]

1. 1. 4. Lengo la jumla la APRM ni kuziwezesha nchi washiriki kuharakisha utumiaji wa vipaumbele na programu za NEPAD katika kufikia malengo na kufuata matendo mema katika maeneo yote ya utawala. Hili linaweza tu kutokea kwa kupitia juhudi za nchi yenyewe kwa

kushirikisha wadau. Lengo hili linahitaji kila nchi, kwa kupitia ushirikishaji mpana unaongozwa na serikali kuandaa Mpango wa Utekelezaji wenye malengo ya muda maalum yatakayowaongoza wadau katika kutekeleza yale yanayohitajiwa na serikali, sekta binafsi, na asasi za kijamii ili kufanikisha dira ya taifa.

1. 1. 5. Hata hivyo, kutokana na tofauti za kihistoria na tofauti za kimaendeleo baina ya nchi, kila nchi itaanzia mahali panapoifaa na nchi zote hazitegemewi kufikia viwango vya juu vya uteklezaji kwa wakati mmoja. Kasi ya maendeleo itategemea kiwango cha kujituma na utashi wa kisiasa wa nchi katika kuchukua hatua za kufanikisha dira yake.

1. 2 Mchakato wa APRM

Tathmini ya APRM itafanywa chini ya uongozi wa Jopo la APRM na usaidizi wa kitaalamu kutoka Sekretariat ya APRM. Tathmini hii inajumuisha hatua tano ambazo zimefasiliwa katika Waraka wa Msingi wa APRM na kujadiliwa kwa kina katika Mwongozo wa Nchi Kujiandaa Kushiriki katika APRM

Hatua ya kwanza ni mchakato wa matayarisho katka ngazi ya Sekretariat ya APRM na ngazi ya taifa husika. Katika hatua hii, Sekretariat ya APRM itatuma hojaji katika nchi zote washiriki kwa kuzingatia malengo, viwango, vigezo na viashiria vilivyokubaliwa. Nchi itajifanyia tathmini kwa kutumia hojaji hii. Nchi pia inatarajiwa kutayarisha Mpango wa Utekelezaji wa awali kwa kutumia sera, programu na miradi iliyopo. Baada ya kupokea tathmini ambayo nchi imejifanyia, Sekretariat ya APRM ambayo kufikia hapo itakuwa imeishaandaa Waraka wa Usuli wa nchi husika kwa kutumia utafiti na taarifa zinazohusiana na nchi hiyo, itatayarisha Makala ya Masuala Muhimu ambayo itaiongoza nchi katika mchakato wa tathmini. Kama kutokana na takwimu zilizopo, Sekretariat ya APRM inaona masuala hayo muhimu yanahitaji tathmini ya kina, itafanya utaratibu utakaoiwezesha asasi nyingine mbia na yenye utaalam wa kutosha kufanya tathmini ya kiufundi. Mwisho wa tathmini ya kiufundi ripoti ya tathmini hiyo itapelekwa kwa Sekretariat na hatimaye kwa Jopo la APRM.

Hatua ya Pili inahusisha ziara ya ujumbe wa APRM katika nchi husika kwa lengo la kufanya majadiliano na wadau wote.

Hatua ya Tatu inahusiana na ujumbe wa APRM uliotumwa katika nchi husika kuandika ripoti. Ripoti hii inatayarishwa kwa kutumia Waraka wa Usuli na Makala ya Masuala Muhimu iliyoandaliwa na Sekretariat ya APRM pamoja na taarifa zilizopatikana wakati ujumbe wa APRM ulipotembelea nchi na kufanya majadiliano na wadau.

Katika **Hatua ya Nne,** ripoti ya ujumbe wa APRM inawasilishwa kwa Sekretariat ya APRM na Jopo la APRM. Baada ya Jopo kuijadili, ripoti hupelekwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili iweze kujadiliwa na hatimaye viongozi hao huorodhesha mambo ambayo yanaonekana muhimu.

Hatua ya Tano ndio hatua ya mwisho katika mchakato wa APRM Hatua hii inajumuisha kutangaza ripoti. Miezi sita baada ya ripoti kujadiliwa na Wakuu wa Nchi zinazoshiriki katika APRM, ripoti itawekwa hadharani na kujadiliwa katika mikutano na vyombo vya kikanda.

1.2.2 Katika mchakato huo kumewekwa awamu ya awali inayojulikana kama **Zoezi la Kuisaidia Nchi**. Dhumuni la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo na msimamo wa pamoja kuhusu falsafa, taratibu, na michakato ya APRM kwa ajili ya kutambua mahitaji ya nchi; kadhalika kunawepo msimamo wa pamoja katika mpango wa shughuli yenyewe na kuisaidia nchi katika maeneo ambako inahitaji msaada.

2. MWONGOZO WA KUJIBU HOJAJI

2. 1. Taratibu za Kujibu Hojaji

2.1.1. Intarajiwa kwamba kabla ya kupokea hojaji, kila nchi itakuwa imeteua Baraza la Taifa la Usimamizi ambalo litakuwa na wawakilishi wa wadau wote kwa lengo la kuratibu mchakato wa APRM.

2. 1. 2 Inategemewa kwamba Baraza la Taifa la Usimamizi wa mchakato wa APRM katika kila nchi litaorodhesha orodha ya wadau wote (serikali, sekta binafsi, asasi za kijamii) ambao watashiriki katika kujibu hojaji hii. Kisha hojaji hii itasambazwa kwa wadau wote kwa kupitia wadau wawakilishi wao waliomo kwenye Baraza la Kitaifa la Usimamizi litaipa Sekretariat ya APRM orodha ya watu wote waliopelekewa hojaaji.

2. 1. 3 Wadau wote watatakiwa kuelekeza nguvu kwenye Sehemu ya Hojaji ambayo inahusiana na utaalam, ujuzi au mamalaka yao lakini watakuwa huru kujibu swali lolote katika sehemu nyingine ambapo wanahamu ya kutoa mchango wao. Wadau wote watatakiwa kutoa nakala ya nyaraka zilizopo na rejea maalum kuhusina na majibu wanayoyatoa ili kukamilisha uhifadhi wa vyanzo mbalimbali vya habari na kuhalalisha majibu yanayotolewa.

2. 1. 4 Wadau wataarifiwa kipindi cha muda ambao wanatakiwa kurudisha hojaji pamoja na ripoti nzima ya tathmini na nyaraka zilziopatikana kwa Kitengo cha Uratibu

2. 1. 5 Kisha Baraza la Taifa la Usimamizi wa APRM litalinganisha majibu yaliyotolewa na ahojiwa na kujadilian na wadau kwa lengo kufikia muafaka kuhusu majibu hayo. Baraza pia litatumia majibu na ripoti mbalimbali za tathmini na tafiti nyinginezo, kuandika Ripoti ya Tathmini Binafsi ya Nchi. Baraza litahakikisha kwamba kila sehemu ya Ripoti ya Tathmini Binafsi ya Nchi ina rejea za kina na kwamba maswali yamejibiwa na viashiria vimeelezewa.

2. 1. 6 Kuhakikisha kwamba kuna ulinganifu na rejea nzuri, kama majibu yatatolewa kwa njia ya electronic, Hojaji inapaswa kujibiwa na wahojiwa wanaoweka majibu yao chini ya swali husika katika Hojaji kwa kutumia waraka huu kama msingi wa kujibia maswali. Wahojiwa hawabanwi katika kutoa majibu yao na wanahamasishwa kutoa maelezo na nyaraka za ziada ili kufafanua majibu yao (Angalia 2. 1. 8 hapa chini).

2. 1. 7 Hata hivyo, kwa kutiia maanani vikwazo vya uwezo mdogo katika kutumia mfumo wa elektroniki kwa baadhi ya wadauu, hojaji nyingine ambayo itawawezesha wadau kujibu kwa kutumia mkono imetayarishwa na Sekretariat na itatumwa kwa Baraza la Taifa la Usimamizi wa APRM kwa ajili ya kuisambaza kwa wadau wanaotaka kujibu kwa kuandika kwa mkono.

2. 1. 8 Pale inapowezekana, wahojiwa wataombwa kuambatanisha nyaraka za kuunga mkono majibu yao. Kwa hiyo, nyaraka hizo zinatakiwa zionyeshwe wazi zinajibu swali gani. Wahojiwa wako huru kutoa rejea toka kwenye mtandao, pale ambapo waraka ambao unatakiwa kuambatanishwa umepatikana kwa njia ya elektroniki.

2. 2. Muundo wa Muhtasari kuhusu Hojaji

2. 2. 1. Juhudi zimefanywa kufanya Hojaji iweze kujibiwa kirahisi. Hojaji ina maelezo kwa muhtasari katika kumrahisishia jukumu mhojiwa

2. 2. 2 Mwanzoni mwa kila sehemu, kuna muhtasari kuhusu sehemu husika na vitu muhimu ambavyo mhojiwa anatakiwa kuvitilia maanani wakati wa kujibu maswali

2. 2. 3 Mwanzoni mwa kila lengo kuna muhtasari wa maelezo ya kuwakumbusha ahojiwa kile kinachotakiwa na mnyumbuliko wa maelezo kuhusiana na maswali na viashiria ili kuwapa nafasi ya kujibu kwa kulingana na mazingira yao.

2. 2. 4 Kwa upande wa maswali na viashiria kuna maelezo ya muhtasari yanayohusiana na viashiria maalum ambavyo vinahitaji uthibitisho.

2. 2. 5 Wahojiwa wanashauriwa kuwasiliana na Baraza la Taifa la Usimamizi ili waweze kupewa ufafanuzi kuhusu namna ya kujibu Hojaji au kueleweshwa kuhusu swali lolote lililomo katika Hojaji. Anuani ya Baraza la Taifa la Usmamizi wa APRM imeonyweshwa katika jarida la Hojaji.

2. 3. Mambo ambayo Yanahusisha Maeneo Mengi (Mambo Mtambuka)

2. 3. 1 Kufuatana na mwelekeo wa NEPAD kuhusu maendeleo, maeneo yenye umuhimu katika Sehemu Nne za Hojaji hayawezi kushughulikiwa kila moja kivyake. Maeneo haya yanatambulika kuwa yenye kuingiliana na yanahitaji kuaonishwa katika kuyashughulikiwa. Muingiliano huu upo katika maeneo mengi lakini kwa madhumuni ya shughuli za APRM, masula yafuatayo yametambuliwa kama masuala yanayotakiwa kupewa umuhimu katika maeneo yote yaliyomo ndani ya Hojaji

- Kuondoa umaskini
- Usawa wa jinsia
- Upelekaji madaraka mikoani
- Uwezo wan chi kushiriki katika APRM
- Upatikanaji na Usambazaji wa habari
- Afya
- Ushiriki mpana
- Uendelevu katika masuala ya fedha, jamii na mazingira

2. 3. 2 Maswali na viashiria kuhusu maswali haya yanayoingiliana yamejengwa na kuingizwa kitaalam kila Sehemu ndani ya Hojaji

2. 3. 3 Inashauriwa kwam,ban chi zihakikishe kwamba wadau wote wanayafahamu haya masuala yanayoingiliana na mengineyo ambayo yanaweza kuwa na umuhimu wa

pekee ndani ya nchi, na kwamba wanakaribishwa kutambua mambo mengine yanayoingliana ambayo wanadhani ni muhimu kwa mtazamo wan chi.

2. 3. 4 Kwa hiyo, nia ni kuzifanya nchi zitayaweka masuala haya katika maeneo yote ya tathmini na kutoa viashiria maalum pale vinapopatikana

2. 4 Maadili na Viwango

2. 4. 1 Ili kutambua mafanikio ambayo yamepatikana katka nchi mojamoja katika kufikia malengo ya kila sehemu iliyomo kwenye hojaji, nchi zinazofanya Tathmini ya APRM zimepitisha viwango na maadili kadhaa na vipimo vinavyotambuliwa kimataifa.

2. 4. 2 Ingawa baadhi ya vipimo hivi vinaweza kuingizwa katika sehemu nne zote za hojaji, vipimo vinavyotumika kwa kila sehemu vimeorodheshwa mwanzoni mwa kila Sehemu.

2. 4. 3 Matokeo yake, swali la kwanza katika kila Sehemu linahusiana na kama nchi inafuata inafuata viwango na maadili yaliyokubaliwa.

SEHEMU YA KWANZA

DEMOKRASIA NA UTAWALA BORA WA KISIASA

Fasili

Utawala Bora maana yake ni kuanzisha asasi za kisiasa, kisheria na kiutawala ambazo zinafanya kazi vizuri na zenye kuwajibika na ambazo raia wanaziona kama vyombo halali vya kuwawezesha na kuwapa fursa ya kushiriki katika kufanya maamuzi ambayo yanahusu maisha yao ya kila siku (Kofi A. Annan, Ubia kwa ajili ya Jumuia ya Kimataifa, (1998)

Demokrasia na Utawala Bora wa Kisiasa ni mojawapo ya masharti muhimu katika kupata mafanikio katika utawala wa kiuchumu, makampuni, na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa sababu mambo haya yanagusa haki za msingi za raia (kama watu binafsi na kama makundi), uwajibikaji wa serikali kwa watawaliwa na utengamano wa mfumo wa utawala kwa ujumla.

Sehemu mojawapo ya msingi katika Azimio la NEPAD ni azma ya Wakuu wa Nchi na Wakuu wa Serikali wa Nchi wanachama wa AU kufanya kazi kwa ari mpya katika maeneo ya:

- Utawala wa Sheria
- Usawa mbele ya sheria na uhuru wa mtu binafsi kujiamulia mambo yake
- Uhuru wa mtu binafsi na makundi ya jamii, ikiwa ni pamoja na uhuru wa kuunda na kujiunga na vyama vya siasa na vyama vya wafanyakazi kwa mujibu wa katiba;
- Usawa wa fursa kwa wote
- Haki zisizoweza za mtu binafsi kushiriki katika michakato ya kidemokrasia katika chaguzi za mara kwa mara na zilizo huru ambaz zinawawezesha kuchagua viongozi wao kila mwisho wa muhula.
- Kufuata hana ya mgawanyo wa mamlaka ikiwa ni pamoja na ulinzi wa uhuru wa mahakama na ufanisi wa Bunge.

1. UTANGULIZI

Sehemu hii ya Hojaji inazngumzia lengo kubwa la APRM ambalo ni ukuzaji wa demokrasia na utawala bora wa kisiasa kama msingi wa kupunguza umaskini na kujiletea maendeleo endelevu.

Kwa hiyo, yamebuniwa maswali yenye lengo la kupima ushiriki wa wananchi na usawa katika mambo ya kisiasa, vitu ambavyo ndio kanuni za jami yenye demokrasia. Maswali haya yamewekwa katika makundi kadhaa.

Mpango wa Uhakika wa Haki Sawa kwa Raia

Kundi hili linajumuisha mambo kama vile fursa ya kupata haki, kuheshimu utawala wa sheria, uhuru wa kutoa maoni, kujiunga na vyama na kutana, pamoja na haki za msingi za kiuchumi na kijamii ili kuwawezesha raia kufaidi uhuru na haki hizi kwa katika namna iliyokusudiwa.

Kuzuia na kupunguza migogoro ya ndani na baina ya nchi, hasa kwa kuangalia namna ambavyo nchi inayofanyiwa tathmini inajitahidi kuendeleza amani na usalama ndani ya mipaka yake na kuchangia kuwepo kwa amani na utengamano katika nchi za irani. Katika hili, kuwepo kwa mfumo wa viashiria vya awali vya migogoro ama vilivyo rasmi au visvyo rami katika nchi au ukanda kunachukuliwa kama jambo la muhimi (Lengo la 1).

Demokrasia ya kikatiba inachukuliwa kama jambo lililotofauti lakini lenye uhusiano na utawala wa sheria. Kwa upande mmoja, demokrasia ya kikatiba inahusiana na kuwepo kwa vifungu vya kikatiba na asasi zinazowawezesha wananchi kufaidi haki na uhuru wa kujiunga na vyama vya siasa wanavyovitaka na kushiriki kwa uhuru kwa vyama hivi na asasi nyingine katika ushindani wa kisiasa. Demokrasia ya kikatiba inawawezesha wananchi katika ngazi za chini kwa kupitia mbinu ya kupeleka madaraka mikoani na ngazi za chini na hivyo kuwafanya wanajumuia kushiriki katika kufanya maamuzi ya mambo yanayohusu maisha yao. Kwa upande mwingine, utawala wa sheria na dhana ya

katiba kama chombo chenye mamalaka ya juu kabisa huhakikisha kwamba watu wanapewa haki sawa kwa mujibu wa seria, na kwamba dola haimtendei mwananchi yeyote kinyume na matakwa ya sheria. Utawala wa Sheria pia unamaanisha kwamba mamlaka zote , ikiwa ni pamoja na majeshi na vyombo vya usalama vinatii sheria. Zaidi ya hapo, sheria na sheria nogo zinazotungwa na serikali zisikiuke katiba ambayo ndiyo sgheria mamam atika nchi na msingi wa mamalka yote ya dola (Lengo la 2).

Ukuzaji wa uhuru wa kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa husaidia kuhakikisha kwamba haki za watu zinaheshimiwa na dola ambayo inatakiwa kuchukua hatua kulinda haki za wananchi ili izisivunjwe na wakala wake au mtu mwingine. Kwa hiyo, suala la kurasimiasha mfumo wa utoaji haki kwa kutumia majaji wenye sifa zinazotakiwa na ambao wanaweza kutafsri sheria bia ya kuogopa shinikizo na bila kupendelea ni la muhimu sana.Viashiria vinavyohusiana na lengo vimeegemea katika kanuni ya kamba ridhaa ya wananchi ndiyo msingi wa mamlaka ya serikali.

Uimarishaji wa Mgaanyo wa mamlaka , ikiwa ni pamoja na ulinzi wa uhur wa mahakama na kulipa Bunge uhuru wa kutosha nayo ni mambo muhimu katika mfumo wa utawala. Lengo hili linahakikisha kwamba kuwepo kwa mfumo mzuri wa mgawanyo wa mamlaka kati ya Mahakama, Bunge na Tawi la Utendaji. Mgawanyo wa Mamlaka hutathmini mfumo wa udhibiti na urari wa mamalaka miongoni mwa matawi ya serikali. Mahakama huru huwapa wananchi, makundi na makampuni imani kwamba haki zao zitalindwa; na pia inasaidia kuletengeza mazingira mazuri ya kuhamasisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Kuwepo kwa Bunge huru na ambalo liko hai katika shughuli zake za udhibiti wa vitendo vya matawi mengine ni muhimu ili kuleta mafanikio katika kupunguza rushwa katika sekta ya umma na matumizi mabaya ya mamlaka ya Tawi la Utendaji (Lengo la 4).

1.2 .Vyombo vya Uwakilishi na Serikali inayowajibika

Sula hili linahusiana na kwepo kwa chaguzi za mara kwa mara na amabzo ni huru na za haki kama njia ya msingi ya kuwawezesha wananchi kushiriki katika kunda

serikali na kufuatilia utendaji wake. Kadhalika suala hili linagusa taratibu za kuwajibika kwa umma kwa viongozi waliochaguliwa na wale ambao sio wa kuchaguliwa. Maswali yanayohsiana na suala hili katika hojaji yanazungmzia malengo makuu mawili.

1.2.1. Kuhakikisha kwamba wale walioko katika ofisi za umma na watumishi wa serikali wanawajibika, wana ufanisi na wanaleta matokeo yanayotakiwa.
Vashiria vilivyoko katika lengo hili vinalenga kutambua kiwango cha ubora wa huduma zinzotolewa na uwajibikaji wa watumishi kwa umma. Utoaji mzuri wa huduma kwa umma huwawezesha wananchi kutoa maoni yao kuhusu utendaji wa serikali na kuwawajibisha watumishi wa serikali (Lengo la 5).

2. Vita dhidi ya rushwa katika siasa. Rushwa hutoa taswira uisiyokuwa saihi ya uchumi wa nchi na hivyo kuwavunja moyo wawekezaji.Katika lengo hili, jaribio linafanywa kuatahmini kiwango cha rushwa nchini na taratibu zilizopo kuzuia vitendo hivyo.

1.3 Asasi za Kijamii zilizohai

Suala hili inajumisha kuwepo kwa vyombo vingi vya habari na asasi zisizokuwa za kiserikali. Sula hili pia linagusa mfumo wa mashauriano katika jamii kwa lengo la kuchochea ushiriki wa wananchi katika mchakat wa kisiaa ikiwa ni pamoja na kuwayahusisha makundi maalum katika kufanya maamuzi, kuifanya serikali kuchukua hatua kuhusiana na maoni ya wananchi na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Msisistizo mkubwa utawekwa katika kuangalia namna wanawake, watoto na makundi mengine maalum kama vile watu aliolazimishwa kuhama kutoka katika maeneo yao ndani ya nchi na wakimbizi wanavyofungamanishwa katika mchakato wa mashauriano ndani ya jamii. Baadhi ya malengo muhimu ambayo ni msingi wa maswali katika hojaji ni:

1. Ukuzaji na ulinzi wa haki za wanawake na kufanya kuingiza suala la usawa wa jinsia katika mipango yote. Hapa suala la msingi ni kuhakikisha hadhi ya wanawake nchini inainuliwa na kutafuta njia za kuongeza ushiriki wao katika masuala ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduini na kijamii, Viashiria katika lengo hili vinakusudia kuishawishi serikali kutoa ushahidi wa uwezeshaji wa wanawake katika kuwawezesha kudhibiti rasilimali za uzalishaji , huduma , na nafasi yao katika kutoa maamuzi ikiwa nui pamoja na kuzuia na kutatua migogoro. Mambo mengine ambayo yanahusiana na wanawake ambayo hayajazungumziwa katika lengo hili yanashughulikiwa kwa upana katika hojaji inayohusiana na Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii.

1.3.2 Ukuzaji na ulinzi wa haki za watoto na vijana. Lengo hili linaangalia zaidi hali ya watoto katika vita, utumwa wa watoto, na matatizo mengine yanayowazuia vijana wasifaidike na mipango ya kukarabati maisha yao (Lengo la 8).

1. 3. 3 Ukuzaji na ulinzi wa haki za makundi maalum ikiwa ni pamoja na watu ambao wamelazimiswa kuhama makazi yao ndani ya nchi na wakimbizi. Kushindwa kuyalinda makundi maalum unaonyesha kushindwa kwa nchi kutumia uwezo wake kwa sababu tu ya ubaguzi wa baadhi ya makundi katika jamii. Maswali yanayoulizwa yanalenga pia kuangalia haki za watu waliolazimishwa kuhama katika maeneo yao na wakimbizi kwa kufunganisha maisha ya makundi hayo na maisha ya jamii kwa ujumla (Lengo la 9).

Kwa vile baadhi ya Viwango na Maadili yansaidia kufasili malengo yaliyoko katika sehemu hii. Ni vivuri mhojiwa akajumuisha orodha ya viwango na maadili ambayo nchi yake imetia saini, imeridhia au inayafuata kwa sasa. Baada ya hapo, mhojiwa anaweza kuendelea kutoa maelezo katika swali la kwanza , huku akitoa ushahidi pale unapohitajika.

Kwa vile sio rahisi kuaoanisha viashiria vya Demokrasia na Utawala wa Kisiasa na vipimo vya uwingi, msisistizo umewekwa kwenye tathmini ya ubora. Haikusudiwi kwamba viashiria vilivyotolewa ni toshelevu. Kwa hiyo katika majibu yako unaweza

kuongeza viashiria vingine ambavyo vinahusiana na nchi yako ambavyo havimo katika hojaji.

Tafadhali kumbuka kwamba kama nchi yako imechukua na kuvitumia viwango vyovyote vya kimataifa ambavyo havimo katika hojaji, uko huru kutoa maelezo kuhusiana na tarehe ya kuchukua viwango hivyo na mipango ya kiasasi iliyowekwa na uwezo wa rasilimali watu na fedha katika kutekeleza viwango hivyo.

2. VIWANGO NA MAADILI

2. 1 Hati Rasmi na Viwango vya Kimataifa

- Mkataba wa Umoja wa Mataifa (kwa malengo yote)
- Azimio la Dunia kuhusu Haki za Binadamu (kwa malengo yote)
- Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (1966) (Lengo la 3)
- Hati za Awali za Mkataba wa Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa (Lengo la 2)
- Azimio la Haki na Uwajibikaji wa Watu Binafsi, Makundi na vyombo vya kijamii kuhusu Ukuzaji na Ulinzi na Haki za Binadamu zinazotambuliwa Dunia nzima: A/RES/53/144 (Lengo la 3)
- Mkataba wa kuzuia Mateso na aina nyingine za Ukatili, Unyama na Kudhalilishwa na Kupewa Adhabu za Kutweza (Lengo la 2).
- Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi (Lengo la 2 na 3).
- Mkataba wa Haki za Kiraia za Wanawake (Lengo la 7)
- Mkataba wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (Lengo la 7)
- Azimio la Kukomesha Vitendo vya Vurugu Dhidi ya Wanawake(Lengo la 7)
- Azimio la Kanuni za Msingi kuhusu Mchango wa Vyom,bo vya Habari kuimarisha Amani na Maelewano ya Kimaifa , Kukuza Haki za Binadamu na Kupambana na Ubaguzi wa Rangi na Uchochezi wa Vita (Lengo la 2 na 3).

- Azimio la Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Kuhusu Migogoro ya Wanawake (Lengo la 1)
- Azimio kuhusu Haki za Watu wa Makundi Madogo ya Kitaifa, Kikabila, Kidini na Kilugha (Lengo la 1, na 3)
- Mkatba wa Kimataifa kuhusu Kulinzi wa Haki za Wafanyakazi Wahamiaji, na Famia Zao (Lengo la 3 na 9)
- Mkataba kuhusu Haki za Watoto (Lengo la 8)
- Itifaki ya Hiari kuhusiana na Mkataba wa Haki za Watoto, inayozungumzia masuala ya watoto kujihusisha katika vita (Lengo la 1 na 8)
- Itifaki ya Hiari kuhusiana na Mkataba wa Haki za Watoto, inayozngumzia a Biashara ya Watoto, Ukahaba miongoni mwa watoto na Picha za Ngono Miongoni mwa Watoto (Lengo la 8)
- Azimio kuhusu Kanuni za kijamii na Kisheria , zinazohusiana na Ulinzi wa Ustawi wa Watoto, kwa kurejea Kulea, Kuwaweka katika makazi na kuasili watoto kitaifa na kitaifa (Lengo la 8)
- Azimio kuhusu Ulinzi wa Watu wote Dhidi ya Mateso na Aina Nyingine za Ukatili, Unyama, na Kudhalilishwa na Kupewa Adhabu za Kutezwa (Lengo la 2 na 3)
- Itifaki ya Hiari kuhusiana na Mkataba Dhidi ya Mateso na Ukatili Meingine, Unyama, Kudhalilishwa na Kupewa Adhabu za Kutezwa.

- Mkataba wa Kupambana na Uuzaji wa Binadamu na Unyonyaji utokano na Kuwatia watu katika Ukahaba I Lengo la 2, 3 na 8)
- Azimio la Kanuni za Msingi za Haki kwa Wahanga wa Uhalifu na Matumizi Mabaya ya Mamlaka (Lengo la 2 na 3)
- Mkataba kuhusiana na Hadhi ya Wakimbizi (Lengo la 9)
- Itifaki kuhusiana na Mkataba wa Hadhi ya Wakimbizi (Lengo la 9)
- Mkataba wa Geneva kuhusu Ulinzi wa Raia wakati wa Vita (Lengo la 2)
- Mkataba wa OECD kuhusu Kupambana na Rushwa miongoni mwa Watumishi wa Umma

- Mkataba wa Kulinda Haki za Wafanyakazi Wahamiaji (ulioanza kutumia Julai 1, 2003) (Lengo la 3)

2. 2 Mikataba na Viwango vya Kikanda

- Sheria ya Awali ya Kuunda Umoja wa Afrika (Malengo yote)
- Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (1990) (lengo la 2, 3, 7, 8 na 9).
- Azimio la Grand Bay (Mauritius) na Mpango wa Utekelezaji kuhusu Ukuzaji na Ulinzi wa Haki za Binadamu (1999) (Lengo 2 na 3)
- Azimio la Durban kuhusu Kanuni zinazotawaa Chaguzi za Kidemokrasia Afrika (2002) (Lengo la 2)
- Azimio la AU kuhusu Utawala katika Demokrasia, Siasa, Uchumi na Makampuni (Lengo la 2, 5 na 6)
- Mkataba wa AU wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Lengo la 5 na 6)
- Itifaki ya AU kuhusu Amani na Usalama (Lengo la 1)
- Mkataba wa AU kuhusu Haki na Ustawi wa Watoto (1990) (Lengo la 8)
- Jukwa la Kiafrika kuhusu Haki ya kupata Elimu (1999)
- Mkataba wa OAU kuhusu Wakimbizi wa 1969 (Lengo la 9)
- Itifaki kuhusu Haki za Wanawake Afrika (2003) (Lengo la 7)
- Azimio la Cairo kuhusu Kuanzishwa Ndani ya OAU, Taratibu za Kuzuia, Kudhibiti na Kutatua Migogoro (1993) (Lengo la 1)
- Makubaliano ya Mkutano kuhusu Usalama, Utengamano, Maendeleo na Ushirikiano Afrika (CSSDCA) Tanko la Dhati (2000) (Lengo la 2)
- Azimio kuhusu Mpango-Sheria wa OAU kushughulikia suala la Mabadiliko ya Serikali yasiyokuwa ya kikatiba (2000) (Lengo la 2)
- Azimio na Mpango wa Utekelezaji kuhusu Kudhibiti Usafirishaji na Utumiaji wa Madawa Haramu Afrika (2000) (Lengo la 1)
- Waraka wa Mpango-Sheria wa NEPAD (Malengo yote)

3. SWALI LINALOHUSIANA NA VIWANGO NA MAADILI

Ni kwa kiasi gani nchi imechukua hatua za kutia saini, kuridhia, kutumia na kufuata viwango hivi kwa ukamilifu?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kutia saini, kuridhia au kukubali mikataba inayohusiana na viwango na maadili.

(ii) Orodhesha hatua zilizochukuliwa kukamilisha zoezi la kuridhia na kufuata maadili na viwango ambavyo vinaonekana kufaa katika mazingira ya nchi yako.

(iii) Eleza kwa muhtasari hatua nyingine za kisheria, kisera au kiasasi ambazo zimechukuliwa ili kutekeleza masuala ambayo yanahusiana na viwango na maadili yaliyoorodheshwa hapo juu kwa namna ambayo inaonekana kukidhi vipaumbele vya nchi yako

(iv) Elezea kwa muhtasari changamoto ambazo zimeonekana na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na mapungufu na uwezo mdogo.

4. TATHMINI ZILIZOPITA

4. 1 Tafadhali toa nakala ya tathmini rasmi zilizokwishafanyika nchini mwako katika uwanja wa **Demokrasia na Utawala wa Kisiasa** ambayo inaweza kuisaidia nchi kujifanyia tathmini.

4. 2 Tafadhali toa nakala ya utafiti kuhusu **Demokrasia na Utawala wa Kisiasa** ambao unadhani utaisaidia nchi kujifanyia tathmini.

5. MASWALI YANAYOHUSIANA NA MALENGO

LENGO LA KWANZA: Kuzuia na kupunguza migogoro ndani na baina ya mataifa

SWALI 1: Kuna migogoro gani inayoendelea nchini mwako na ni vipi vyanzo vyake?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha vyanzo vya migogoro ambayo inaonekana inaweza kuathiri amani, utengamano, na usalama (vyanzo vya ndani ya nchi), ikiwa ni pamoja na yafuatayo:

- Usafirishaji wa madawa ya kulevya
- Uhalifu unaopangwa na makundi ya wahalifu
- Tofauti za kiuchumi na mgawanyo wa utajiri
- Biashara haramu ya silaha
- Tofauti za kikabila, kidini na nyinginezo
- Wakimbizi na watu waliolazimishwa kuhama toka sehemu moja kwenda nyingine ndani ya nchi.

(ii) Orodhesha vyanzo vikuu vya migogoro baina ya nchi yako na nchi jirani

SWALI 2: Kuna utaratibu gani ulioweka wa kuzuia, kupunguza, na kudhibiti migogoro katika nchi yako au ukanda wako na ni kwa kiasi gani taratibu hizo zimeleta matokeo yanayotakiwa?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa juhudi iliyofanywa na nchi yako hasa kwa kuangalia vifungu vya sheria, asasi na ugawaji wa rasilimali katika kukabiliana na tofauti za kikanda, kidini, kutokuwepo kwa usawa kiuchumi na nyinginezo;

(ii) Elezea juhudi zilizofanywa na nchi yako katika kuendeleza mahusiano ya amani na majirani zake, ikiwa ni pamoja na kusimamia mipaka yake na kutatua migogoro inayohusiana na mipaka

(iii) Toa usahidi wa kuwepo kwa mfumo wa viashiria vya awali na utaratibu mwingine ambao umewekwa kushughulikia migogoro ndani na baina ya mataifa;

(iv) Tathmini kama taratibu zilizopo zinaleta matokeo yanayotakiwa na hatua zilizochukuliwa kulinda mafanikio yaliyopatikana katika udhibiti wa migogoro na baada ya migogoro (usimamizi, tathmini, na ufuatiliaji) .

Karibuni: inamaaniasha katika kipindi cha miaka 5-10 iliyopita . Lakini tafsri hii inaweza kuchukuliwa vinginevyo kulingana na historioa ya nchi.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI 3: Ni kwa kiasi gani mashirika ya kikanda yanajihusisha na utatuzi wa migogoro ya ndani ya nchi au migogoro baina ya mataifa ambayo inaathiri nchi yako?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha asasi za kikanda zilizo hai katika utatuzi wa migogoro katika nchi yako, ukitoa mifano ya migogoro ambayo asasi hizo zimejihusisha au kutatua;

(ii) Tathmini ufanisi wa asasi hizi katika kuzuia na kudhibiti migogoro na kuiumarisha amani, usalama na utengamano;

(iii) Elezea changamoto ambazo asasi hizo zimekumbana nazo katika utatuzi wa migogoro na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

LENGO LA PILI: Demokrasia ya kikatiba, ikiwa ni pamoja na ushindani wa kisiasa wa mara kwa mara, fursa ya kuchagua, utawala wa sheria, haki za raia na dhana ya katiba kama mamlaka ya juu kabisa.

SWALI 1: Kwa mawazo yako, mfumo wa siasa kama unavyoendeshwa nchini mwako unaruhusu kuwepo kwa ushindani ulio huru na wa haki katika kugombea madaraka na kuendeleza utawala wa kidemokrasia?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha haki za kisiasa za mtu binafsi na za kijamii na taratibu na asasi zilizowekwa kulinda haki hizo;

(ii) Orodhesha vifungu vya sheria na taratibu zinazohusiana na uhuru wa kujiunga na vyama vya siasa katika nchi yako;.

(iii) Pima ufanisi wa vifungu na taratibu hizo katika kuimarisha vyama vya siasa na hususan katika suala la uanachama, sera na ugawaji wa rasilimali kwa vyama vya siasa katika nchi yako;

(iv) Elezea mfumo wa uchaguzi katika nchi yako, ukitaja vifungu vya kisheria na kikatiba vinavyohusika;

.

(v) Pima ufanisi wa mfumo wa uchaguzi wa nchi yako hasa kwa kuangalia uwezo wake wa kutoa matokeo ambayo kwa ujumla wake yanaonekana kuwa huru na ya haki;

(vi) Onyesha ripoti kutoka katika vyanzo vya serikali na vinginevyo kuhusu uchaguzi uliofanyika hivi karibuni nchini mwako;

(vii) Toa ushahidi kuhusu kesi za uchaguzi zenye mvutano mkali za hivi karibuni na jinsi zilivyoamuliwa na mahakama.

Karibuni: inamaaniasha katika kipindi cha miaka 5-10 iliyopita. Lakini tafsri hii inaweza kuchukuliwa vinginevyo kulingana na historioa ya nchi.

SWALI 2: Kivitendo, vifungu vinavyohusiana na utawala wa sheria na dhana ya katiba kama mamlaka ya juu kabisa, vinapewa uzito gani?

VIASHIRIA

(i) Onyesha vifungu vya sheria ambavyo vinajenga utawala wa sheria na kuimarisha dhana ya katiba kama mamlaka ya juu kabisa na elezea taratibu za kurekebisha katiba ya nchi yako;

(ii) Orodhesha asasi zilizopewa jukumu la utekelezaji wa vifungu hivi na pima ufanisi wa asasi ukitumia kesi au ripoti za hivi karibuni

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 3: Ni kwa namna gani na kwa kiasi gani suala la upelekaji wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda ngazi za chini linafanyika nchini mwako?

VIASHIRIA

(i) Onyesha vifungu vya sheria vinavyohusika na upelekaji wa madaraka ngazi za chini na uhuru uliopo katika vyombo hivyo vya chini;

(ii) Pima ufanisi wa utaratibu wa kupeleka madaraka ngazi za chini hasa katika suala la kufanya maamuzi, ugawaji wa rasilimali, uwezo wa kiasasi, utoaji wa huduma; na uorodheshe hatua zilizochukuliwa kushughulikia udhaifu uliojitokeza katika taratibu hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 4: Upelekekaji wa madaraka kutoka serikali kuu kwenda ngazi za chini umesaidiaje kuboresha utawala?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi unaonyesha kwamba upelekaji wa madaraka kutoika serikali kuu kwenda ngazi za chini umeongeza kiwango cha ushiriki na ushirkishwaji wa wananchi katika ngazi hizo;

(ii) Toa ushahidi unaoonyesha kuwepo kwa uwajibikaji katika asasi ambazo zimepelekewa madaraka katika ngazi za chini.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 5: Je, vyombo vya ulinzi na usalama vinawajibika kwa utawala wa sheria na kwa vyombo vya kiraia vya udhibiti wa mamlaka?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya kisheria na taratibu za uwajibikaji wa vyombo vya ulinzi na usalama kwa vyombo vya kidemokrasia vya serikali, hasa Mahakama na Bunge/Baraza la Wawakilishi;

(ii) Pima ufanisi wa vyombo vya kiraia vya udhibiti wa mamlaka katika suala la bajeti na matumizi ya vyombo vya ulinzi na usalama;

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA TATU:Ukuzaji na ulinzi wa haki za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa kama ilivyokubaliwa katika maazimio ya nchi za Kiafrika na Jumuia za Kimataifa kuhusu haki za binadamu

SWALI LA 1: Hatua gani zimechukuliwa katika kukuza na kulinda haki za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia na kisiasa?

VIASHIRIA

(i) Onyesha vifungu vya sheria ambavyo vinatambua na kulinda haki mbalimbali ikiwa ni pamoja na haki ya:

- Usawa katika kujipatia ajira
- Elimu
- Afya
- Uhuru wa kuzungumza
- Uhuru wa kuabudu
- Kupata malazi nafuu kwa mwananchi wa kawaida

(ii) Pima ufanisi wa vifungu vya sheria na taratibu zinazokuza na kulinda haki;

(iii) Toa ushahidi unaoonyesha kesi kubwa za uvunjaji wa haki na uhuru wa raia ambazo zimeshughulikiwa na mahakama katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Hatua gani zimechukuliwa kuhakikisha kwamba kunakuwepo na fursa sawa kwa watu wote katika kutafuta haki mahakamani?

VIASHIRIA

(i) Onyesha ushahidi wa vifungu vya sheria, asasi na taratibu zilizowekwa kuhakikisha kwamba watu wanapata fursa ya kwenda kutafuta haki mahakamani, ukionyesha ada zinazotozwa, umbali wa kufika ilipo mahakama, elimu kuhusu sheria na msaada wa kisheria unaopatikana;

(ii) Toa maelezo ya kina kuhusu utatuzi mbadala wa migogoro (kama upo) ambao unafanya kazi nchini mwako;

(iii) Toa maelezo ya kina kuhusu hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana (mafunzo, usimamizi, tathmini na marekebisho) katika uwanja huo wa fursa sawa katika kutafuta haki mahakamani.

(iv) Toa ushahidi wa tathmini yoyote rasmi iliyofanywa huko nyuma (katika kipindi cha miaka 5-10) katika mfumo wa utoaji haki ili kujua kiwango cha watu wanaopata nafasi ya kwenda kutafuta haki mahakamani.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA NNE: Kuimarisha mgawanyo wa mamlaka, ikiwa ni pamoja na kulinda uhuru wa Mahakama na Bunge kufanya yale yanayotakiwa.

SWALI LA 1 : Kuna vifungu gani vya kisheria na kikatiba ambavyo vinaweka mgawanyo wa mamlaka na udhibiti wa mamlaka miongoni mwa matawi ya serikali ambayo ni Tawi la Utendaji, Bunge na Mahakama.

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya kisheria na kikatiba vinavyoweka na kulinda mgawanyo wa mamlaka;

(ii) Elezea utaratibu (kama upo) wa kutatua migogoro baina ya matawi haya ya serikali;

(iii) Pima ni kwa kiasi gani mgawanyo wa mamlaka na taratibu za udhibiti na urari wa mamlaka vimeleta matokea yanayotakiwa;

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi wa migogoro iliyojitokeza na jinsi ilivyotatuliwa

SWALI LA 2: Mahakama iko huru kwa kiasi gani?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya kisheria unaoonyesha kuwepo kwa uhuru wa mahakama, ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa rasilimali na taratibu za uteuzi, usalama wa ajira, upandishaji vyeo, maslahi, na mambo yanayohusiana na nidhamu na adhabu kwa maofisa wa mahakama;

(ii) Pima kiwango cha uhuru wa mahakama kilichopo na toa ushahidi kuunga mkono makadirio hayo;

(iii) Toa maelezo ya kina kuhusu ripoti yoyote rasmi ya tathmini au utafiti uliofanywa huko nyuma kuhusu uhuru wa mahakama.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 3: Kwa maoni yako, unadhani Bunge/Baraza la Wawakilishi lina uhuru kiasi gani?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya kisheria na mgawanyo wa rasilimali unaoonyesha uhuru wa Bunge/Baraza la Wawakilishi; ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa miswada, kupendekeza marekebisho ya sheria (ikiwa ni pamoja na marekebisho ya bajeti), na fursa ya kuhoji vitendo vya Tawi la Utendaji;

(ii) Pima kiwango cha uhuru wa Bunge/Baraza la Wawakilishi na toa malezo ya kina kuhusu ripoti yoyote rasmi inayozungumzia makadirio ya uhuru huo.

(iii) Elezea hatua zilizochukuliwa kulinda mafanakio ya uhuru wa Bunge (mafunzo, tathmini, ripoti zilizopo).

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA TANO: Kuhakikisha kwamba walioko katika ofisi za umma na watumishi wa serikali wanawajibika, wana ufanisi na wanaleta matokeo yanayotakiwa

SWALI LA 1: Hatua gani zimechukuliwa nchini mwako kuimarisha asasi kwa lengo la kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unakuwa na ufanisi na wenye kuleta matokeo yanayotakiwa?

VIASHIRIA

(i) Toa maelezo ya kina kuhusu vifungu vya sheria, taasisi na mgawanyo wa rasilimali ambao unalenga kuleta ufanisi na kuhakikisha kwamba utumishi serikalini unaleta matokeo yanayotakiwa;

(ii) Toa ushahidi wa marekebisho ya kiutawala yaliyofanywa kuboresha utoaji wa huduma katika utumishi wa umma na hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio;

(iii) Elezea taratibu za kukuza tabia ya kufanya tathmini ya utoaji huduma katika utumishi wa serikali ikiwa ni pamoja na fursa ya raia kutoa maoni yao kuhusu ubora wa huduma zinazotolewa.

(iv) Toa ushahidi kuunga mkono tathmini yako ikiwa ni pamoja na ripoti yoyote rasmi inayohusiana na ufanisi na bidii za kuleta matokeo yanayotakiwa katika utoaji wa huduma katika utumishi wa umma

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Ni kwa kiasi gani nchi imejenga mfumo wa uwazi katika uajiri, mafunzo, upandishaji vyeo, utawala na tathmini ya watumishi wa serikali?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha vifungu vya kisheria, taratibu na asasi zinazohusika na uajiri, upandishaji vyeo, utawala na tathmini ya watumishi wa serikali;

(ii) Toa ushahidi wa vivutio vinavyotumika kuwapa motisha watumishi wa serikali wanaotekeleza majukumu yao vizuri;

(iii) Toa ushahidi wa kesi zinazohusiana na masuala ya adhabu za kinidhamu, ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi na kushitakiwa kwa watumishi wa serikali kuhusiana na mapungufu katika utoaji wa huduma;

(iv) Toa ushahidi wa hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana (usimamizi, tathmini na mafunzo).

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA SITA: Vita dhidi ya rushwa katika siasa

SWALI LA 1: Rushwa imefikia kiwango gani nchini mwako?

VIASHIRIA

(i) Pima hisia za jumla za kuwepo kwa rushwa katika nchi yako

(ii) Toa ushahidi kuunga mkono makadirio yako ikiwa ni pamoja na ripoti rasmi kuhusu kiwango cha rushwa nchini

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Hatua gani zimechukuliwa na mambo gani yamefanywa kupambana na rushwa katika siasa na yapi matokeo ya mapambano hayo?

VIASHIRIA

(i) Elezea hatua za kisheria na kiasasi ambazo zimechukuliwa kupambana na rushwa, ikiwa ni pamoja na suala la kutangaza mali, kuundwa kwa vyombo

maalum vya kupambana na rushwa na taratibu za uteuzi wa wakuu wa vyombo hivyo;

(ii) Toa maelezo ya kina kuhusu kesi kubwa zinazohusiana na rushwa ambazo zimepelekwa mahakamani na adhabu zilizotolewa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA SABA: Ukuzaji na ulinzi wa haki za wanawake

SWALI LA 1: Hatua gani zimechukuliwa kukuza na kulinda haki za wanawake nchini mwako?

VIASHIRIA

(i) Toa maelezo ya kina kuhusu vifungu vya kisheria vinavyoonyesha na kulinda haki za wanawake nchini na taratibu za kutekeleza haki hizo ikiwa ni pamoja na mgawanyo wa rasilimali, nafasi za upendeleo na kuweka dhana ya usawa wa jinsia katika programu na mipango ya nchi;

(ii) Pima ni kwa kiasi gani hatua hizi zimeleta matokeo yanayotakiwa na elezea kwa muhtasari changamoto zilizojitokeza;

(iii) Elezea kwa kina hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana (mafunzo, tathmini na usimamizi);

(iv) Toa ripoti yoyote rasmi inayopima nafasi ya wanawake nchini mwako

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWAL LA 2: Hatua gani zimechukuliwa kuongeza ushiriki wa wanawake katika masuala ya jamii?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya sheria, asasi na programu za kitaifa au ngazi za chini, au sera zinazosaidia kuboresha nafasi ya wanawake katika jamii, ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika siasa na nafasi za uongozi;

(ii) Toa ushahidi wa idadi na asilimia ya wanawake walioteuliwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kushika nafasi za kufanya maamuzi ikiwa ni pamoja na idadi ya wanawake waliochaguliwa katika chaguzi za Wabunge na serikali za mitaa;

(iii) Elezea changamoto zilizopatikana na hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA NANE: Ukuzaji na ulinzi wa haki za watoto na vijana

SWALI LA 1 : Hatua gani thabiti zimechukuliwa kukuza na kulinda haki za watoto na vijana

VIASHIRIA

(i) Toa maelezo ya kina kuhusu vifungu vya sheria, hatua na sera ambazo zinakuza na kulinda haki za watoto na vijana ikiwa ni pamoja na haki zifuatazo:

- Afya, matunzo na ustawi
- Elimu kwa watoto
- Uangalizi na malezi ya watoto
- Haki ya kutafuta na kupokea habari kwa lengo la kukuza ustawi wa kijamii, kiroho, kimwili na kiakili

- Hatua zilizochukuliwa dhidi ya aina zote za ukatili dhidi ya watoto ikiwa ni pamoja na utumwa wa watoto, ajira za watoto, ukahaba miongoni mwa watoto, na picha ngono miongoni mwa watoto.

(ii) Pima ufanisi wa hatua hizi kwa kuangalia uboreshaji wa hali za watoto na vijana nchini katika kipindi cha miaka mitano ilioyopita;

(iii) Toa ushahidi wa hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana (mafunzo, usimamizi, ufuatiliaji, marekebisho, na ripoti zilizopo)

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA TISA: Ukuzaji na ulinzi wa haki za makundi maalum katika jamii ikiwa ni pamoja na wakimbizi na watu waliolazimishwa kuhama makazi yao ndani ya nchi.

SWALI LA 1: Nchi imechukua hatua gani kukuza na kulinda haki za makundi maalum ikiwa ni pamoja na wakimbizi na watu waliolazimishwa kuhama makazi yao ndani ya nchi.

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa vifungu vya kisheria, asasi na mgawanyo wa rasilimali ambavyo vinasaidia kukuza na kulinda haki za makundi maalum katika jamii na wakimbizi, ikiwa ni pamoja na programu za ukarabati, afya, elimu, makazi, na juhudi za kuyachanganya na kuyashirikisha makundi hayo katika shughuli zote za kijami;

(ii) Pima ufanisi wa hatua hizo na toa maelezo ya kina kuhusu uvunjaji wa haki hizo na ripoti inayoweza kupatikana kuhusiana na jambo hilo.

(iii) Toa maelezo ya kina kuhusu hatua zilizochukuliwa kuendeleza mafanikio yaliyopatikana (usimamizi, mafunzo, ufuatiliaji na marekebisho).

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SEHEMU YA PILI

UTAWALA WA KIUCHUMI NA UONGOZI

Fasili

Katika Azimio la Demokrasia na Utawala wa Kiuchmi na Kisiasa, nchi za Kiafrika zilitambua kwamba “utawala mzuri wa uchumi ikiwa ni pamoja na uwazi katika usimamizi wa fedha ni masharti uya muhimu katika kuhamasisha ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini.”

Ni imani thabiti ya wakuu wa Nchi na Wakuu wa Serikali za nchi za Umoja wa Afrika (AU) kwamba kuwepo kwa ufanisi katika masoko , udhibiti wa matumizi mabaya , na uimarishaji wa demokrasia na uwingi wa mitaji binafsi ni mambo muhimu katika jitihada za kupunguza umaskini na kuleta maendeleo endelevu barani Africa.

1. UTANGULIZI

Matataizo ya Afrika kwa kwa ujumla yanachukuliwa kama mgogoro wa kisiasa wenye athari za kiuchumi. Ni vizuri ikakumbukwa kwamba matatizo ya uchumi ya nchi za Afrika katika miongo iliyopita itakuwa imechochewa na machafuko ya kisiasa na hivyo kuzidi kuathiri hali ya maisha ya wananchi wengi wa Afrika.

Matatizo hayo ya uchumi yanaathiri masuala ya ndani ya nchi na vilevile masuala ya nje ya nchi. Masuala haya ni pamoja na ukusanyaji mdogo wa mapato na kutegemea misaada; kuwepo kwa benki kuu dhaifu na sekta za fedha zisizokuwa na ufanisi; kutokuwepo kwa uwazi katika masuala ya bajeti, kutokuwepo kwa udhibiti wa Bunge na vyombo vingine wenye ufanisi; mazingira yasiyofaa kwa wawekezaji binafsi na yanayotawaliwa na rushwa; miundombinu dhaifu; na utawala usiotabirika.

Lengo la kwanza la Usimamizi wa Uchumi na Fedha za Umma ni kukuza utengamano wa sera za msingi za uchumi ambao unachukuliwa kama kigezo muhimu kwa upande wa maendeleo endelevu. Hata hivyo, kutengamana kwa sera za msingi za uchumi peke yake hakutoshi kuboresha hali za maisha ya watu. Kwa upande mwingine, usimamizi wa uchumi na fedha hakuwezi kuleta maendeleo endelevu kama sera zinazotekelezwa hazina uwazi na haziaminiki ndani na nje ya nchi. Kwa hiyo, ili kushughulikia jambo hili Hojaji ya Utawala katika Uchumi na Uongozi inahusiana zaidi na mambo yafuatayo:

- Kuhamasisha kuwepo kwa sera za msingi za uchumi ambazo zinachochea maendeleo endelevu
- Kutekeleza sera za uchumi zilizo wazi, zinazoaminika na zinazotabirika;
- Kuhamasisha kuwepo kwa usimamizi mzuri wa fedha za umma
- Kuongeza kasi katika ushirikiano wa kikanda kwa kuoanisha sera za kifedha na uwekezaji miongoni mwa nchi wanachama wa ushirikiano wa kikanda.

Ili kuweza kufahamu mafanikio yaliyokwishapatikana katika kufikia malengo haya, nchi zinazoshiriki katika Mpango wa Kujifanyia Tathmini (APRM) zimepitisha Viwango na

Maadili ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na: Maadili ya Matendo Mema na Uwazi katika Masuala ya Sera za Fedha; Maadili ya Matendo Mema kuhusu Usimamizi wa Fedha za Umma; Maadili ya Matendo Mema katika Uwazi wa Bajeti; Taratibu katika Usimamizi wa Deni; na Kanuni za Msingi katika Usimamizi wa Mabenki.

Kutokana na hali hiyo, kipengele cha kwanza katika Hojaji ni swali linalohusiana na namna nchi inavyofuata maadili na viwango vilivyokubaliwa. Baada ya hapo, maswali mengine yanazungumzia hatua zinazochukuliwa na nchi kufikia malengo matano yaliyotajwa, na athari ya hatua hizo. Maswali ya msingi yanahusu mambo yafuyatyo:

- Ubora wa sera za msingi za uchumi
- Sera za kisekta zinazohamasisha maendeleo endelevu
- Ufanisi na uwazi wa utawala wa umma
- Uwezo wa kiasasi
- Upelekaji wa madaraka kuhusu mambo fedha katika ngazi za chini za mamlaka;
- Hatua za kupambana na rushwa na mzungusho wa fedha haramu;
- Hatua za kuendeleza ushirikiano wa kikanda na ushirikiano katika mambo ya fedha

Viashiria kadhaa vimetolewa kusaidia kujibu maswali yaliyoulizwa katika sehemu hii. Katika baadhi ya maeneo tathmini inafanywa kwa kutumia vigezo vya uwingi. Kwa mfano, ubora wa sera za msingi za uchumi unapimwa kwa vigezo vya uwingi kama vile wastani wa mfumko wa bei kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita; Ukuaji halisi wa Pato la Taifa katika kipindi cha miaka5 iliyopita; Ulipaji wa madeni, na Nakisi katika bajeti. Katika maeneo mengine, hojaji inatoa vigezo vya kiubora ili kufahamu vizuri mchanganyiko wa masuala, ikiwa ni pamoja na tathmini za vitu kama ufanisi na uwazi katika utawala wa umma, ubora katika usimamizi wa fedha za umma, na ufanisi katika kupeleka madaraka yanayohusiana na mambo ya fedha ngazi za chini.

Hata hivyo, katika baadhi ya maeneo, ikiwa ni pamoja na uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali, hojaji imetengenezwa katka hali ambayo inajumuisha vigezo vya uwingi na vigezo vya ubora. Kwa mfano, ubora wa sera za kisekta za nchi unatathiminiwa sio tu kwa

kulinganisha uzalishaji halisi na ukuzaji wa ajira kwa kila sekta katika kipindi cha miaka 5 iliyopita, bali pia kwa kuoanishwa na hatua zinazochukuliwa kukuza usawa wa jinsia, uendelevu wa mazingira na jamii na kuongeza nafasi za ajira.

Tafadhali jibu kila swali na viashiria vilivyotajwa. Viashiria vya ziada ambavyo vinaonekana muafaka vinaweza kutumika. Tafadhali andika chanzo ambacho kinaweza kuthibitisha majibu yako. Kwa upande wa vigezo vya uwingi, tafadhali andika thamani ya kitakwimu ya kila kigezo. Kwa upande wa vigezo vya ubora, tafadhali toa maelezo mafupi lakini yaliyo fasaha. Katika vigezo vyote viwili, toa maelezo ambayo yanaonekana kuwa ya muhimu na rejea ya chanzo cha takwimu

Tafadhali jibu swali la kwanza linalohusiana na viwango na maadili yaliyoorodheshwa. Tafadahali jisikie kuwa huru kuongeza viwango na maadili ambayo hayakujumuishwa katika orodha hii.

2. VIWANGO NA MAADILI

- Waraka wa Mpango-sheria wa NEPAD [2001]
- Sheria ya Kuanzisha Umoja wa Afrika (2000)
- Maadili ya Matendo Mema kuhusu Uwazi wa Matumizi ya Umma
- Mwongozo kuhusu Usimamizi wa Madeni ya nchi
- Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Mahesabu
- Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu
- Maadili ya Matendo Mema kuhusu Uwazi wa Masmbo ya Fedha
- Kanuni za Mfumo wa Malipo
- Kanuni za Msingi za Ufanisi katika Usimamizi wa Mabenki
- Mkataba wa Umoja wa Afrika kuhusu Kuzuia na Kupambana na Rushwa
- Mkataba wa Abuja wa kuanzisha Jumuia ya Uchumi ya Afrika (1991)
- Matendo Mema katika Uwazi wa Bajeti
- Kanuni za Utawala wa Makampuni (za kitaifa na kimataifa)
- Mikataba na Protokali kuhusu Jumuia za Kiuchumi za Kikanda

3. SWALI LINALOHUSIANA NA VIWANGO NA MAADILI

SWALI: Ni kwa kiasi gani nchi imechukua hatua za kutia saini, kuridhia, kutumia na kufuata viwango hivi kwa ukamilifu?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi kuhusu utiaji saini, kuridhia au kukubali viwango na maadili hayo;

(ii) Elezea hatua za kisheria, sera, programu, maendeleo ya kiasasi, na mgawanyo wa rasilimali, ambazo nchi imechukua kutumia, kutekeleza na kufuata viwango hivyo kwa ukamilifu;

(iii) Elezea mafanikio yaliyopatikana katika kufikia viwango au malengo kwa kuangalia matokeo;

(v) Orodhesha changamoto ambazo zimeonekana na hatua zilizochukuliwa kusahihisha mapungufu na matatizo ya ya uwezo mdogo.

4. TATHMINI ZILIZOPITA

4.1 Tafadhali toa nakala ya tathmini rasmi iliyofanyika nchini mwako katika eneo la **Utawala wa Kiuchumi na Uongozi** ambayo inaweza kuisaidia nchi kujifanyia tathmini.

4. 2 Tafadhali toa nakala yoyote ya utafiti na uhakiki kuhusu **Utawala wa Kiuchumi na Uongozi** ambao unadhani utaisaidia nchi kujifanyia tathmini.

5. MASWALI YANAYOHUSIANA NA MALENGO

LENGO LA KWANZA: Kukuza sera za msingi ma za ujumla za kiuchumi ambazo zinachochea maendeleo endelevu (Angalia angalizo hapa chini)

Angalizo: Hojaji kuhusu Maendeleo ya Kiuchumi naKijamii ina maswali ya kina kuhusu hatua zilizochukuliwa na mafaniko yaliyopatikana katika suala la maendeleo endelevu. Kwa hiyo, sehemu hii inalenga zaidi kuangalia kama kuna kulandana kwa sera za uchumi na madhumuni ya NEPAD kuhusu maendeleo endelevu.

SWALI 1: Ni kwa kiasi gani sera za msingi za uchumi zinaonekana kuwa nzuri na zinazounga mkono maendeleo endelevu?

VIASHIRIA

(i) Tathmini maendeleo ya sera za msingi za uchumi katika nchi yako ukitilia maanani viashiria vifuatavyo:

- Wastani wa mwenendo katika mfumko wa bei;
- Ukuaji halisi wa Pato la Taifa (GDP) kwa kila mtu katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;
- Ulipaji wa deni kama sehemu ya mapato ya nchi, kiwango cha deni la ndani kama sehemu ya deni la jumla, deni la jumla kama sehemu ya pato litokanalo na kuuza bidhaa nje, na deni la jumla kama sehemu ya PatolaTaifa (GDP);
- Nakisi ya bajeti kama sehemu ya Pato la Taifa (GDP);
- Sehemu ya nakisi katika bajeti inayojazwa kwa kutumia fedha kutoka Benki Kuu kwa miaka 5 iliyopita;
- Sehemu ya bajeti inayopelekwa kwenye huduma za jamii;

- Mikopo kwa sekta binafsi na sekta ya umma katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;

(ii) Elezea hatua zilizochukuliwa na nchi kuhakikisha kwamba sera za msingi za uchumi ni nzuri na zinachochea maendeleo endelevu ikiwa ni pamoja na hatua za kutathmini, kufuatilia na kujua athari ya sera hizo;

(iii) Orodhesha changamoto kubwa zitokanazo na sera za msingi za uchumi, sababu za kujitokeza changamoto hizo na hatua zilizochukuliwa kukabiliana nazo.

Viashiria vya ziada vinaweza kutumika ili mradi viwe vinahusiana na tathmini ya sera za msingi za uchumi katika nchi yako.

SWALI LA 2: Serikali hutunga sera za msingi za uchumi kwa kufuata misingi gani?

VIASHIRIA

(i) Elezea (kwa ufupi) mchakato na njia zinazotumika kutunga sera za msingi za uchumi;

(ii) Toa ushahidi wa ufanisi wa mchakato na njia hizo hasa kwa kuzingatia yafuatayo:

- Tofauti za makisio ya viashiria muhimu vya sera za msingi za uchumi kwa miaka mitano iliyopita;

- Kiwango cha kufikiwa makisio ya sera za msingi za uchumi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;
- Utoshelevu na kuaminika kwa takwimu za sera za msingi za uchumi;

(iii) Iwapo makisio ya sasa ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa (GDP) na mapato ya serikali kwa mwaka ujao ni makubwa kuliko ukuaji halisi wa uchumi katika miaka 5 – 10 iliyopita, toa sababu;

(iv) Elezea ni kwa kiasi gani serikai inakubali ushauri wa tathmini huru ya mwelekeo wa sera za msingi za uchumi wa kitaifa, na toa ripoti yoyote ya mtu au chombo huria kuhusu mwelekeo wa namna hiyo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 3: Nchi yako imebuni na kutekeleza sera gani za msingi za uchumi au sera za kisekta kwa lengo la kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha sera za kisekta, sera za msingi za uchumi, na programu ambazo zilikubaliwa na kutekelezwa katika kuchochea maendeleo endelevu;

(ii) Elezea hatua zilizochukuliwa katika kuhakikisha kuwa kuna usawa wa jinsia, mazingira endelevu na upatikanaji wa ajira katika sera na proramu za kisekta na sera za za msingi za uchumi;

(iii) Toa ushahidi wa mafanikio yaliyopatikana kuelekea kwenye maendeleo endelevu hasa katika viashiria vifuatavyo:

- Ukuaji wa ajira kwa kila sekta kwa miaka 5 iliyopita;
- Uzalishaji katika sekta muhimu za uchumi kwa miaka 5 iliyopita;
- Viashiria vya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ikiwa ni pamoja na masuala ya afya, elimu, HIV/AIS na makazi;

Viashiria vya ziada vinaweza kutumika ili mradi viwe vinahusiana na tathmini ya sera za msingi za uchumi katika nchi yako.

SWALI LA 4: Nchi yako imefanya nini kuongeza ukusanyaji wa rasilimali za ndani ikiwa ni pamoja na akiba ya sekta ya umma na binafsi, uundaji wa mtaji na upunguzaji wa uvushaji wa mitaji kwenda nje ya nchi?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha hatua muhimu za kisheria, sera, programu na maendeleo ya kiasasi ambazo zimechukuliwa katika kukuza ukusanyaji wa rasilimali za ndani, na kuongeza msaada wa kifedha;

(ii) Tathmini ufanisi wa hatua hizi hasa ukizingatia

- M2/ GDP;
- Mapatao yatokanayo na bajeti kama sehemu ya Pato la Taifa;
- Wastani wa akiba ya sekta binafsi na sekta ya umma kama sehemu ya Pato la Taifa ya Taifa (GDP) kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita;

.

- Uundaji wa mitaji kama kama sehemu ya Pato la Taifa kwa mika 5 iliyopita;
- Idadi ya wananchi wanaopata fursa ya kupata mitaji ikiwa ni pamoja na mitaji midogo na taasisi za kuweka akiba, kulinganisha na idadi ya wananchi wote nchini;

(iii) Orodhesha changamoto zilizopatikana na hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 5: Nchi yako ni dhaifu kiasi gani katika kukabiliana na mitikisiko ya kiuchumi kutoka ndani na nje ya nchi?

VIASHIRIA

(i) Elezea kiwango na kujirudia kwa mitikisiko iliyojitokeza katika uchumi katika kipindi cha miaka 5 iliyopita hasa kuhusiana na viashiria vifuatavyo:

- Kiwango cha kubadilika urari baina ya uagizaji wa bidhaa na mauzo ya bidhaa nje ya nchi
- Hatua kuhusu aina za bidhaa zinazouzwa nje na zile zinazoagizwa toka nje;
- Masharti ya biashara kwa miaka 5 iliyopita;
- Mabadiliko katika rasilimali halisi za nje

(ii) Orodhesha hatua zilizochukuliwa kupunguza udhaifu wa nchi yako katika kukabiliana na mitikisiko ya kiuchumi kutoka ndani na nje ya nchi;

Viashiria vya ziada vinaweza kutumika ili mradi viwe vinahusiana na tathmini ya sera za msingi za uchumi wan chi yako.

LENGO LA PILI:Utekelezaji wa mipango ya uchumi mizuri, iliyo wazi na inayotabirika

SWALI LA 1 : Nchi yako imefanya nini kuhakikisha kwamba utawala wa umma, mfumo wa utungaji sheria na mamlaka zinazohusiana na mambo ya fedha zinafanya kazi kwa ufanisi na kwa uwazi ?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha hatua muhimu za kisheria, sera, programu, maendeleoa ya kiasasi na ugawaji wa rasilimali unaosaidia vyombo vilivyotajwa hapo juu kufanya kazi wa ufanisi na kwa uwazi;

(ii) Toa ushahidi wa ufansi na uwazi wa vyombo hivi hasa katika viashiria vifuatavyo:

- Kusambaza habari kuhusu shughuli za vyombo hivyo kwa wakati unaofaa, kwa upana na kwa kurudia mara nyingi;

- Kuwepo kwa taratibu, ikiwa ni pamoja na sheria, katika kufanya tathmini ya ndani na nje ya shughuli za vyombo hivi;

(iii) Orodhesha changamoto kubwa kuhusiana na uwazi na ufanisi wa vyombo hivi na elezea juhudi zilizofanywa kushughulikia changamoto hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Nchi yako imechukua hatua gani kufanya sera za uchumi ziweze kutabirika ?

VIASHIRIA

(i) Onyesha vifungu na michakato iliyowekwa kuhakikisha kwamba kuna ushiriki na ushirikishwaji wa wadau wote katika utungaji wa sera;

(ii) Elezea mchakato ambao umekubaliwa katika kutunga na kufuatilia utekelezaji wa sera za uchumi;

(iii) Elezea hatua zilizochukuliwa kuhakikisha kwamba wananchi wanafahamishwa sera za msingi za uchumi, utekelezaji wake na mafanikio yake;

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

SWALI LA 3 : Ni zipi changamoto kubwa ambazo nchi yako inakabiliana nazo kuhusiana na uratibu wa juhudi za idara mbalimbali katika kutekeleza sera za uchumi ambazo ni nzuri, zilizo wazi na zenye kutabirika ?

VIASHIRIA

(i) Elezea (kwa ufupi) vifungu vya kisheria vinavyoonyesha ushirkiano baina ya idara za serikali na mamlaka za ngazi za chini katika kutekeleza sera za uchumi na programu katika ngazi ya taifa na ngazi za chini;

.

(ii) Tathmini hali ya sasa ya uratibu na uwezo ambao umefikiwa katika idara husika katika kutekeleza sera za uchumi ambazo ni nzuri, zilizo wazi na zenye kutabirika hasa katika maeneoyafuatayo:

- Uhamishaji wa haraka na unaoaminika wa fedha kutoka makao makuu ya mamlaka zinazohusika na utoaji fedha kwenda katika mawizara na wakala maalum;

- Ni mara ngapi miradi na programu za umma zinatelekezwa;

- Uwezo wa wizara na wakala maalum katika kutumia fedha wanazoletewa

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

LENGO LA TATU: Kuhamasisha kuwepo kwa usimamizi mzuri wa fedha za umma

SWALI LA 1: Nchi yako imefanya nini kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa fedha za umma?

VIASHIRIA

(i) Onyesha hatua muhimu zilizochukuliwa (kwa maana ya sheria, sera, programu, ukuzaji wa asasi na ugawaji wa rasilimali) katika kutekeleza mwongozo wa kifedha unaotabirika kuhusu malengo ya muda wa wastani;

(ii) Tathmini hali ya sasa ya usimamizi wa fedha za umma kwa kuangalia yafuatayo:

- Matumizi na mapato halisi ya walengwa katika bajeti ya kila mwaka kwa miaka 5 iliyopita;

- Kiwango cha uwajibikaji wa serikali kwa wafuatiliaji na utoaji wa ripoti kuhusu mapato na matumizi kwa umma;
- Muundo wa mjadala wa wazi na kazi za vyombo vya udhibiti wa fedha za serikali katika ngazi ya taifa ;

- Muda unaotolewa kwa Bunge kupitia na kupitisha makadirio ya bajeti;

- Idadi ya marekebisho yaliyofanywa na Bunge katika rasimu ya makadirio ya bajeti;

(iii) Orodhesha changamoto zilizojitokeza katika kupitisha na kutekeleza mwongozo wa kifedha wa muda wa wastani na juhudi za kukabiliana na changamoto hizo.

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

SWALI LA 2: Nchi yako imechukua hatua gani kubuni mpango wenye ufanisi katika kupeleka ngazi za chini madaraka yanayohusiana na mambo ya fedha?

ANGALIZO: Suala linalozungumziwa katika hojaji ya Utawala wa Kiuchumi ni upelekaji wa madaraka yanayohusiana na fedha katika ngazi za chini. Hojaji ya Utawala wa Kidemokrasia na Kisiasa ina maswali zaidi kuhusiana na hatua zilizochukuliwa kuleta ufanisi katika upelekaji wa madaraka ngazi za chini. Hojaji kuhusu Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii inaliangalia suala la upelekekaji wa madaraka ngazi za chini kwa kulenga katika ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

VIASHIRIA

(i) Elezea (kwa ufupi) vifungu ya kisheria na sera vinavyoweka mfumo wa upelekaji wa madaraka ngazi za chini kwa kuangalia uhusiano baina ya mamlaka ya kitaifa na yale ya ngazi za chini;

(ii) Tathmini ufanisi wa mfumo huu kwa kuangalia yafuatayo:

- Kiwango cha kushabihiana kwa sera na programu zilizoanzishwa na mamlaka za chini na changamoto za mandeleo katika eneo husika;

- Uwezo wa mamlaka za ngazi za chini kujipatia rasilimali za kifedha (kama inawezekana), kupanga na kutekeleza sera za kiuchumi;

- Orodhesha changamoto muhimu zilizojitokeza nchini katika utekelezaji mfumo wenye ufanisi wa kupelekeka madaraka ngazi za chini.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA NNE: Vita dhidi ya rushwa na mzungusho wa fedha haramu

ANGALIZO: Rushwa katika usimamizi wa shughuli za umma inajumuisha kasoro katika matumizi ya fedha za umma, ikiwa ni pamoja na kasoro katika manunuzi katika sekta ya umma na manunuzi mengineyo, au hongo katika utoaji wa huduma kwa umma. Rushwa katika uwanja wa siasa inashughulikiwa katika hojaji ya Utawala wa Kidemokrasia na Kisiasa, na rushwa inayohusiana na mashirika ya umma na mashirika ya watu binafsi inashughulikiwa katika Hojaji ya Utawala katika Makampuni.

SWALI LA 1: Rushwa imefikia kiwango gani katika utawala wa umma katika nchi yako na hatua gani zimechukuliwa katika eneo hili?

VIASHIRIA

(i) Elezea (kwa ufupi) chanzo cha na ukubwa wa rushwa katika utawala wa umma;

.

(ii) Toa ushahidi kuhusu maendeleo yaliyopatikana katika vita dhidi ya rushwa kwa kuangalia vigezo vifuatavyo:

- Kuwepo kwa vifungu vya sheria vinavyoweka taratibu za wazi na zinazotekelezeka za manunuzi katika sekta ya umma;

- Kuwepo kwa vifungu vya sheria na maadili ya kitaifa ya watumishi wa serikali, ikiwa ni pamoja na kutangaza mali;

- Kesi za rushwa katika sekta ya umma ambazo zimeshughulikiwa na Tume inayoshughulikia malalamiko ya rushwa, Kamati ya Bunge ya Fedha za Serikali, au chombo kingine katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;

- Ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kupeleka mahakamani kesi zinazohusina na rushwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita;

(iii) Orodhesha changamto muhimu zilziozojitokeza katika vita dhidi ya rushwa katika utawala wa umma na juhudi zilizofanywa kushughulikia changamoto hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Mzungusho wa fedha haramu unafanyika kwa kiwango gani nchini mwako?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha hatua muhimu za kisheria, sera, programu, ukuzaji wa asasi, na mgawanyo wa rasilimani katika kupambana na vita dhidi ya mzungusho wa fedha haramu;

(ii) Toa ushahidi wa mafanikio yaliyopatikana katka kujenga uwezo wa kupambana na mzungusho wa fedha haramu hasa kwa kuzingatia yafuatayo:

- Vitendo vinavyohusiana na mzungusho wa fedha haramu katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;

- Ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kupelekea mahakamani kesi zinazohusiana na mzungusho wa fedha haramu katika kipindi cha miaka 5 iliyopita;

(iii) Orodhesha changamoto zilizopatikana katika kupambana na mzungusho wa fedha haramu na juhudii za kushughulia changamoto hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina na viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi vema mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini.

LENGO LA TANO : Kuongeza kasi ya ushirikiano wa kikanda kwa kuoanisha sera za kifedha, kiuchumi na vitega uchumi

SWALI LA 1: Nchi yako ni mwanachama wa ushirikiano wowote wa kiuchumi wa kikanda na nini faida na changamoto za uanachama huo? (kama sio, tafadhali nenda swali namba 2 la lengo la 5)

VIASHIRIA

(i) Taja mwaka ambapo nchi yako iliingia rasmi katika ushirikiano wa kikanda na taja jina la ushirikiano huo ambao nchi yako ni mwanachama;

(ii) Toa tathmini fupi ya faida za nchi yako kushiriki katika ushirikiano huu wa kiuchumi wa kikanda;

.

(iii) Orodhesha changamoto na mafunzo yatokanayo na kushiriki katika ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

SWAL LA 2: Hatua gani ambazo nchi yako imechukua kuhakikisha kwamba sera

za kitaifa, ikiwa ni pamoja na sera za biashara na ukuzaji wa uwekezaji baina ya nchi za Afrika zinashabihiana na kuunga mkono malengo ya kiuchumi ya ushirikiano wa kikanda?

VIASHIRIA

(i) Elezea (kwa ufupi) sera za uchumi za kitaifa ikiwa ni pamoja na zile zinazohusu biashara na ukuzaji wa uwekezaji baina ya nchi za Afrika;

(ii) Toa tathmini ya kiwango ambacho sera za kitaifa za uchumi zinashabihiana na kuunga mkono malengo ya ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda katika maeneo yafuatayo:

- Kushabihiana baina malengo ya sera za kitaifa na malengo ya sera za ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda;
- Ukuaji wa biashara baina ya mataifa ya Afrika;
- Kukua kwa uwekezaji vitega uchumi baina ya mataifa ya Afrika

(iii) Orodhesha changamoto muhimu zilizojitokeza na mafunzo yaliyopatikana.

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

SWALI LA 3 : Kuna hatua gani ambazo nchi yako imechukua kuhakikisha kwamba kuna utekelezaji wenye ufanisi wa maamuzi na makubaliano yanayofanywa katika ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha hatua zilizochukuliwa kwa upande wa sheria, sera, ukuzaji wa asasi, uratibu, ujenzi wa uwezo, na mgawanyo wa rasilimali katika kuhakikisha kwamba utekelezaji wa maamuzi na makubaliano yaliyofikiwa katika ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda unakuwa na ufanisi;

(ii) Tathmini wepesi katika kuyakubali na kutekeleza maamuzi na makubaliano ya ushirikiano wa kiuchumi wa kikanda katika ngazi ya taifa nchini mwako;

(iii) Orodhesha vizuizi vinavyokwamisha ujenzi wa uwezo na jitihada zilizofanywa kuondoa vikwazo hivyo.

Viashiria vya ziada vinaweza kuongezwa ili kuakisi vema mazingira na uzoefu maalum uliopo nchini

SWALI LA 4: Je, nchi yako imechukua hatua gain kukuza juhudi za ushirikiano wa kikanda hasa katika masuala ya kuoanisha na kuratibu masuala ya fedha?

VIASHIRIA

(i) Orodhesha hatua za kisheria, sera, ukuzaji wa asasi, ujenzi wa uwezo na mgawanyo wa rasilimali katika kuimarisha juhudi za kuoanisha na kuongeza ushirikiano na uratibu wa mambo ya fedha;

.

(ii) Tathmini mafanikio yaliyopatikana katika ushirikiano wa kikanda katika kufuata makubaliano, mikataba, na protokali kuhusu kuoanisha, kushirikiana na kuratibu mambo ya fedha;

(iii) Orodhesha faida na changamoto zilizojitokeza na elezea hatua zilizochukuliwa kushughulikia vikwazo vilivyojitokeza.

Tafadhali toa maelezo ya kina na viashiria vya ziada vionaweza kuongezwa ili kuakisi vema mazinira na uzoefu maalum ulioo nchini.

SEHEMU YA TATU

UTAWALA KATIKA MAKAMPUNI

Fasili

Utawala wa Makampuni ni mfumo utumiwao kuongoza, kudhibiti na kuwajibisha makampuni na mashirika. Unahusisha mambo yote yahusuyo uendeshaji katika makampuni binafsi na mashirika ya umma.

Utawala Bora wa Makampuni huruhusu kiasi fulani cha uwazi kuhusiana na jinsi yanavyoendeshwa, bodi zao za wakurugenzi, na kuleta usimamizi wa uwajibikaji unaohakikisha kwamba makampuni: yanawajibika kisheria na kutoa mafao/kodi; yanawajibika kwa wanahisa na wadau kwa ujumla wakiwamo wafanyakazi, wazabuni, wkopeshaji; walaji na wanajamii kwa juml; na yanawajibika kuhusiana na mazingira.

Utawala Bora wa Makampuni una sifa bainifu saba: nidhamu, uwazi, uhuru, uwajibikaji, majukumu, usawa katika kutoa haki, na uwajibikaji kijamii. Sifa hizi ni muhimu kwa sababu zinaongeza imani ya wawekezaji, jambo linaloyawezesha makampuni kupata mitaji na fedha nyinginezo za kuendesha shughuli zao. Afrika ni bara ambalo kihistoria limevutia uwekezaji mdogo sana. Inasadikiwa kuwa utawala bora wa makampuni utabadili hali hii na kuvuta wawekezaji wa ndani na nje na hasa kama utawala bora utapanuliwa na kuhusisha suala la uendeshaji mzuri wa uchumi kwa jumla. Zaidi ya hilo, nchi nyingi za Afrika zinategemea kilimo, madini na rasilimali nyingine za aina hiyo ambazo uendelezaji wake una madhara kwa mazingira. Kama vile hiyo haitoshi, umaskini wa kutupa, njaa, na majanga ya maradhi kama ukimwi, malaria na kifua kikuu vyote vinazinyemelea jamii zetu. Hii ina maana kuwa dhana ya “kampuni kama raia mwema” na uwajibikaji wa makampuni kijamii inatakiwa kuzingatiwa kama tunataka makampuni yasituharibie mazingira na watu wafaidike kutokana na kuwepo kwa makampuni miongoni mwao

1. UTANGULIZI

Dira ya NEPAD ni kuondoa umaskini na kuziweka nchi za Afrika kwa pamoja au mojamoja katika mwelekeo wa maendeleo na ukuaji endelevu. Hili linahitaji kuwepo uzalishaji mali endelevu na ukusanyaji wa utajiri kupitia asasi zinazotawaliwa vizuri –

ziwe za binafsi au za umma. Ili kuwe na utawala bora wa makampuni, Wakuu wa Nchi na Wakuu wa Serikali waliafiki maazimio makuu matano na viwango na maadili yatakayoongoza maboresho ya utawala wa makampuni.

Kutengeneza mazingira na mipango-sheria ya kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika

Lengo hili linatilia mkazo hatua za kisheria na kiutawala zinazowezesha shughuli za kiuchumi kufanyika bila bughudha. Uchambuzi wa awali wa kipemgele hiki unalenga kutathmini ufanisi wa vyombo vya serikali (hasa katika mabenki, bima, na soko la mitaji) na mamlaka zinazojiendesha zenyewe (soko la hisa, vyama vya kitaaluma na vyama vya kibiashara) katika kudhibiti, kuangalia na kusimamia shughuli.

Majadiliano kuhusiana na lengo hili hadi sasa yamekuwa yakilenga zaidi masuala ya amani na usalama, ufanisi wa vyambo vya mahakama na waendesha mashtaka ikiwa ni pamoja na polisi, maendeleo ya miundombinu na rasilimali watu kama ndio mambo yanayoathiri shughuli za kiuchumi. Kama ilivyokwishaelezwa, kuna maeneo manne ambayo APRM inayaangalia ikiwa ni pamoja na Demokrasia na Utawala wa Kisiasa na Maendeleo ya Kijamii na Uchumi ambayo yanaangalia masuala haya kwa kina. Katika sehemu hii tunataka kuangalia kwa undani ni mambo gani yanaathiri ufanisi wa sekta ya biashara ikiwa ni pamoja na uhuru katika maamuzi, uwezo na ufanisi wa mahakama katika kusimamia sheria za biashara, mawasiliano ya uhakika na upatikanaji wa habari, na kuwepo kwa rasilimali watu bora inayohusiana na uendeshaji wa makampuni kama vile wahasibu, wakaguzi wa mahesabu, wanasheria, makatibu wa makampuni, na kadhalika.

1. 2 Kuhakikisha kuwa makampuni yanakuwa ‘raia’ wema kuhusiana na haki za binadamu, kuwajibika kijamii, na kuweka mazingira endelevu

Lengo hili lina mambo makuu matatu: haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kuheshimu sheria za kazi, kuwajibika kijamii, na mambo yanayohusu mazingira.

Baadhi ya mambo yaliyoangaliwa kwa undani hapa ni pamoja na: haki za waajiriwa, kuweka mazingira salama ya kufanyia kazi na ujira wa haki; kiwango cha usikivu wa makampuni kwa masuala na mahitaji ya kijamii ikiwemo yale ya afya [Ukimwi, malaria, kifua kikuu na homa ya manjano], elimu na uendelezaji wa elimu ya amali; na kujiheshimu kuhusiana na suala la mazingira ikiwamo miradi ya kukarabati mazingira, tathmini za athari kwa mazingira, kutumia tena vitu vilivyotumika na kutumia teknolojia safi.

1.3 Kuhamasisha kuwepo kwa maadili mema ya kibiashara katika makampuni kufikia malengo

Ripoti ya King II inafasili maadili ya biashara kuwa ni “miongozo, maadili na viwango vinavyoongoza taasisi kuendesha mambo yake, mahusiano ya ndani na mahusiano yake na wadau walio nje ya taasisi yenyewe”. Chini ya lengo hili, baadhi ya vigezo vitakavyoangaliwa ni kujisimamia na kujiandalia maadili ya hiari ya namna ya kuendesha shughuli katika makampuni/mashirika ya binafsi na yale ya umma, na kuheshimu na kutekeleza miongozo na maadili haya.

Mambo mengine yanayoangaliwa hapa ni pamoja na mbinu za kuwaadhibu wale wanaokiuka maadili na ufanisi wake. Jambo jingine linaloangaliwa ni upatikanaji wa habari kuhusu makampuni na uhuru wa waandishi wa habari na ubora wa habari za fedha na uchunguzi au habari nyinginezo zinazolinda “maslahi ya umma”.

1. 4 Kuhakikisha kuwa makampuni yanawatendea haki wadau wakiwemo wana hisa, waajiriwa, wanajamii na wazabuni

Lengo hili linakusudia kuangalia dhana ya makampuni kuwajibika kwa wanahisa na majukumu yao kwa wadau. Maswali yanagusa maeneo kama haki za wanahisa ikiwa ni

pamoja na kuhamisha, kuuza au kabadili hisa, kupata habari sahihi kuhusu kampuni kwa wakati na kila zinapohitajika, kushiriki kupiga kura katika vikao vya kuchagua wakurugenzi wa bodi, kupata sehemu ya faida inayopatikana, na ni kwa namna gani mwanahisa anaweza kudai haki zake endapo zitavunjwa na kampuni. Ingawa baadhi ya haya hayahusu mashirika ya umma, masuala ya uwajibikaji na ufanisi katika huduma za kiuchumi zinazotolewa na mashirika ya umma yanapaswa kuzingatiwa.

Katika kipengele hiki pia kuna suala la sheria na maadili ya mahusiano baina ya wadau na makampuni kwa mfano vyama vya wafanyakazi, sheria ya walaji, haki za wakopeshaji na sheria ya mufilisi, na jinsi zinavyozingatiwa katika nchi.

Mfano wa tabia inayoweza kuonyesha kampuni inavyowatendea wadau ni pamoja na kurudisha bidhaa zenye kukosa viwango, matangazo yasiyo na ukweli, wauzaji kula njama za kupanga bei, haki ya wafanyakazi kugoma, kiwango cha makampuni kufilisika, malalamiko toka kwa wanajamii na kadhalika.

1. 5 Kuhakikisha kuna kuwajibika kwa makampuni, wakurugenzi na maafisa

Lengo la kipengele hiki ni kupima ufanisi wa mfumo wa utawala wa kampuni katika shuruti ya kutoa habari, utekelezaji wake na fidia aipatayo mhusika endapo miongozo imekiukwa. Mfano hapa ni ukaguzi wa mahesabu, uhasibu na uhifadhi wa rekodi za kampuni kwa mujibu wa viwango vya kimataifa, muda unaohitajika kupata habari za kifedha za kampuni, na programu za mafunzo kwa wakurugenzi na maofisa.

2. VIWANGO NA MAADILI

- Waraka wa Mpango-sheria wa NEPAD [2001]
- Kanuni za Utawala wa Makampuni (OECD na Jumuia ya Madola)

- Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Mahesabu
- Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu
- Kanuni za Msingi za Usimamizi thabiti wa Mabenki
- Mkataba wa Nchi za Kiafrika Kuhusu Haki za Watu
- Maadili ya Kazi ya ILO
- Kanuni za Msingi za Usimamizi na Taratibu za Dhamana na Bima
- Maadili ya Usafi na Usalama wa Mazingira na Viwanda ya Shirika la Afya Duniani

3. SWALI LINALOHUSU VIWANGO NA MAADILI

SWALI: Ni kwa kiasi gani nchi imechukua hatua za kusaini, karidhia, kutumia na kufuata kwa ukamilifu viwango hivi?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kutia saini, kuridhia, au kuvikubali viwango hivi pale vinapotumika;

(ii) Ni hatua gani zinachukuliwa kukamilisha zoezi la kuridhia na kufuata viwango hivyo?

(iii) Kama nchi yako haijaridhia viwangona maadili hayo hapo juu, kuna sheria, sera, au miongozo ipi mingine inayoongoza mambo ya makampuni nchini?

(iv) Onyesha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kusahihisha mapungufu na matatizo ya uwezo mdogo

(v) Elezea maendeleo yaliyopatikana katika kufikia viwango au malengo kwa kutumia vipimo muafaka.

4. TATHMINI NA MAKADIRIO YA HUKO NYUMA

4.1 Tafadhali toa nakala za tathmini na makadirio ambayo nchi yako ilishawahi kufanya katika suala la Utawala wa makampuni ambayo yatasaidia nchi yako kujitathmini.

4. 2 Tafadhali toa nakala za tafiti nyingine zilizowahi kufanyika katika eneo hilo la Utawala wa Makampuni ambazo wewe unaona zitasaidia katika kutathmini nchi yako.

5. MASWALI YANAYOHUSU MALENGO

LENGO LA KWANZA: Kutengeneza mazingira na mpango-sheria imara wa kuwezesha shughuli za kiuchumi kufanyika.

SWALI LA 1: Ni yapi makundi makuu ya makampuni ya kibiashara na yana wajibu gani katika uchumi wa nchi?

VIASHIRIA

(i) Tafadhali elezea makundi makuu ya makampuni ya kibiashara kuhusiana na:

- Aina tofauti za makampuni, umiliki wake na majukumu yake katika uchumi yakiwamo makampuni ya umma yaliyoandikishwa kwenye soko la hisa, makampuni binafsi yaliyoandikishwa kwenye soko la hisa, makampuni ya serikali, vyama vya ushirika makampuni ya kifamilia, sekta isiyo rasmi na kadhalika.

- Historia, ukubwa na utendaji wa masoko ya hisa (kama yapo).

(ii) Orodhesha taasisi za kifedha zinazoshirikiana na kusaidia sekta ya biashara nchini zikiwamo benki, ushirika wa ujenzi , wakala wa serikali, mipango ya uwekezaji, vyombo vya fedha vya kimataifa, vyombo vya mikopo midogo midogo n.k.

(iii) Tafadhali toa orodha ya vyombo vya uwekezaji vya ndani kama makampuni ya hifadhi ya jamii, vyama vya kuweka na kukopa, benki, bima; wawekezaji wa nje na kiasi cha uwekezaji na kushiriki kwao katika mfumo rasmi wa kifedha;

(iv) Orodhesha vyama vya kitaaluma na kitaalam na kibiashara kama vyama vya wenye viwanda, vyama vya wazalishaji, chama cha wakurugenzi na chama cha wahasibu waliobobea.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Kuna mfumo gani wa udhibiti wa shughuli za kiuchumi na ni kwa kiasi gani unayasaidia makampuni ya kibiashara nchini?

VIASHIRIA

(i) Elezea kwa kifupi mfumo wa sheria na udhibiti unaotumika katika kuongoza makampuni ya kibiashara, ikiwa ni pamoja na makampuni yaliyoandikishwa katika soko la hisa, makampuni ambayo hayakuandikishwa katika soko la hisa, mashirika ya umma, na asasi za kifedha;

(ii) Kama kuna soko la hisa, eleza kinachotakiwa ili kampuni iweze kuandikishwa, ukionyesha hatua za mwanzo na baada ya kuandikishwa inatakiwa ifanye nini;

(iii) Toa maelezo ya kina ni mamlaka zipi zina jukumu la kusimamia masuala ya kibiashara katika nchi ikiwa ni pamoja na mamlaka inayosimamia masoko ya mitaji;

(iv) Tathmini ufanisi na kufaa kwa asasi hizo za usimamizi kuhusiana na:

- Utaratibu wa kufuata katika usajili, kutoa leseni na kufutiwa usajili wa makampuni mbalimbali, na uonyesha kama kuna tofauti zozote.

- Kueleweka na kufungamana kwa sheria zinazoongoza mwenendo wa makampuni, ikiwa ni pamoja na sheria ya makampuni, sheria za kazi, sheria ya kodi, sheria ya mufilisi, na nyinginezo;

- Ufanisi wa mahakama na vyombo vingine vya udhibiti katika kutatua migogoro ya kibiashara na kuyashtaki makampuni yenye kukiuka sheria;

- Ubora na ufanisi wa vyombo vya usimamizi vya serikali (hasa mabenki, bima, masoko ya dhamana) na vyombo vya kujidhibiti wenyewe (ikiwa ni pamoja na masoko ya hisa, vyama vya kitaaluma) katika udhibiti, uangalizi na usimamizi.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika.

SWALI LA 3: Ni mambo gani ya nje na ndani yanaathiri shughuli za kibiashara?

VIASHIRIA

(i) Elezea hali ya miundombinu iliyo katika nchi kama barabara, teknohama, upatikanaji na kuaminika kwa nishati, n.k.

(ii) Elezea juhudi zinazofanywa na nchi kuhamasisha shughuli za biashara ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji, kuanzisha vijikampuni, kuanzisha makampuni madogo, kuanzisha makampuni ya kati, ubinafsishaji, kugeuza asasi za umma kuwa za asasi za kibiashara, kanuni za masoko ya mitaji,

uuzaji usio na vikwazo wa hisa, na juhudi za kanzisha makampuni maalum kama yale ya wanawake, makampuni yasiyo rasmi n.k.

(iii) Orodhesha changamoto zinazozikumba shughuli za kiuchumi nchini na juhudi zinazofanywa kukabili changamoto hizo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA PILI: Kuhakikisha kuwa makampuni yanakuwa 'raia' wema kuhusiana na haki za binadamu, kuwajibika kijamii, na kuweka mazingira endelevu

Angalizo: Hojaji ya Demokrasia na Utawala wa Kisiasa ina maswali mengi ya haki za binadamu kwa hiyo hapa tunaangalia zaidi sheria ya kazi na haki za wafanyakazi mahali pa kazi

SWALI LA 1: Je kuna hatua za kuhakikisha kuwa makampuni yanazingatia haki za binadamu na haki za kazi?

VIASHIRIA

(i) Elezea sheria za kazi za nchi yako hususan kuhusiana na;

- Haki za mwajiriwa ikiwepo haki ya kujiunga na chama cha wafanyakazi,
- Utaratibu wa kusuluhisha migogoro ya kazi;

(ii) Tathmini jinsi makampuni yanavyofuata sheria za kazi na haki za binadamu hususan kuhusiana na:-

- Kuwepo kwa mazingira salama ya kufanyia kazi na mshahara wa haki,

- Makampuni yanavyoshughulikia migogoro ya kikazi, masuala ya usalama na mambo yahusianayo na fidia kwa wafanyakazi, ikiwemo fidia ya kuumia ukiwa kazini,

- Idadi ya vyama vya wafanyakazi, asilimia ya wafanyakazi walio wanachama wa vyama hivyo, na ufanisi wa vyama vya wafanyakazi katika kushughulikia migogoro ya kikazi,

- Mara ngapi kumekuwepo na migogoro ya kikazi na migomo mikubwa ,

- Rejea makampuni yaliyofikishwa mahakamani kwa kosa la kuvunja haki za binadamu na adhabu yalizopewa.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika.

SWALI LA 2: Ni kwa kiasi gani makampuni ni sikivu na yanaweka maanani masuala na kero za jamii yanakofanyia shughuli zake?

VIASHIRIA

(i) Eleza ni kwa kiasi gani makampuni yanashiriki kwenye shughuli za kijamii za kimaendeleo ukitilia maanani:

- Kiwango cha makampuni yanayojihusisha moja kwa moja na shughuli za kijamii katika maeneo yanakofanyia shughuli zake na michango yao katika ajenda na vipaumbele vya maendeleo katika ngazi ya taifa k.m. ukimwi, usawa wa jinsia, kupunguza umaskini, kuongeza ajira na kuendeleza utaalam na ujuzi wa aina mbalimbali n.k.;

- Kuwepo kwa ushirikiano wa sekta mbalimbali (ikiwa ni pamoja na makampuni, serikali, na jamii) katika kutunga sera za kuendesha mambo ya umma.

(ii) Toa mifano ya miradi na programu zilizofadhiliwa na makampuni kama sehemu ya uwajibikaji wake kwa jamii;

(iii) Pima kiwango cha uwajibikaji kijamii wa makampuni yaliyoko nchini kwa kuangalia mambo yafuatayo:

- Kujihusisha kwa makampuni katika utekelezaji wa maadili ya kuwajibika kijamii na kiwango cha utoaji wa taarifa kuhusu masuala ya kimaadili na ya kijamii,

- Mlandano wa miradi ya kuwajibika kijamii iliyoanzishwa na makampuni na mahitaji ya jamii ,

- Kiasi cha makampuni kuwakera wanajamii kutokana na shughuli zake na idadi ya malalamiko dhidi ya shughuli za makampuni;

- Mashirika (zikiwamo AZISE na asasi nyingine za kijamii) yanayozungumzia na kuhimiza agenda ya uwajibikaji kijamii wa makampuni na maslahi muhimu yanayopiganiwa;

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 3: Ni hatua zipi zimechukuliwa kuhakikisha kuwa makampuni yanajihusisha na mazingira katika hali ya uendelevu?

VIASHIRIA

(i) Kwa kifupi eleza uzoefu wa nchi yako kuhusiana na uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za makampuni;

(ii) Toa ushahidi wa kuwepo sheria, sera, programu, asasi na rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kulinda mazingira;

(iii)Tathmini ufanisi wa hatua hizi kuhusiana na:

- Kwa kiasi gani makampuni yanatekeleza sera zihusuzo uhifadhi endelevu wa mazingira ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, utumiaji wa teknolojia safi isiyoharibu mazingira, kutumia tena vitu vilivyokwisha tumika (recycling) na programu za kukarabati mazingira;

- Idadi ya marejeo ya kesi za makampuni yaliyoshitakiwa kuhusiana na kuharibu mazingira, na ni adhabu zipi yalipewa, na ni kwa vipi kanuni ya "anayechafua mazingira afidie makosa yake" inatekelezwa;

- Kwa kiasi gani makampuni yanatoa taarifa kuhusiana na athari ya shughuli zao katika mazingira na hasa makampuni yanayovuna maliasili kama vile wachimba madini na wazalishaji viwandani;

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA TATU: Kuhamasisha kuwepo kwa maadili mema ya kibiashara katika kufikia malengo ya kampuni

Angalizo: Sehemu inayozungumzia Utawala katika Uchumi inaangalia mambo

kama mzungusho wa fedha haramu na rushwa katika sekta ya utawala. Rushwa katika siasa inashughulikiwa katika sehemu ya Demokrasia na Utawala wa Kisiasa. Sehemu hii inaangalia tu mambo yanavyoathiri mashirika ya umma na makampuni binafsi.

SWALI LA 1: Hali ya ujumla ya uadilifu wa makampuni nchini ikoje?

VIASHIRIA

(i) Onyesha hatua zilizokwishachukuliwa ili kukuza maadili mema ya kibiashara ikiwa ni pamoja na:

- Kuunda maadili ya matendo mema yanayoweza kuigwa katika sekta binafsi na ya sekta ya umma, matumizi yake na jinsi yanavyotekelezwa;

- Hatua za kupambana na uhalifu usiokuwa wa sulubu, ikiwa ni pamoja na biashara inayofanyika baada ya kupata siri za ndani ya makampuni, rushwa na mzungusho wa fedha haramu;

- Jukumu la vyombo vya habari na ubora wa habari za kiuchunguzi na mambo ya fedha katika kuanika wazi makosa ya jinai ya kiuchumi na uvunjaji wa maadili;

- Programu za mafunzo kwa wataalamu kama vile wahasibu, wanasheria, na wakurugenzi ili wawe na viwango vinavyotakiwa kuhusiana na maadili.

(ii) Onyesha ni asasi zipi za kiserikali na za sekta binafsi zimekuwa zikipigania kuwepo kwa maadili mema katika biashara nchini mwako (kwa mfano, Chama cha Wakurugenzi, Kituo cha Utawala wa Makampuni, au Chama cha Wanahisa) na kwa kifupi eleza mada za juhudi za hivi karibuni (kama zipo) katika kuhamasisha biashara nchini;

(iii)Tathtmini kufaa kwa hatua zilizopo katika kujaribu kuleta maadili mema katika biashara hususan kuhusu:

- Ufanisi wa vyombo vya udhibiti ikiwemo usimamizi kupitia vyama vya kitaaluma;

- Mafanikio katika kuendesha kesi zinazohusiana na rushwa, mzungusho wa fedha haramu, kufanya biashara baada ya kupewa siri za ndani ya kampuni, na aina nyingine za uvunjaji wa maadili na adhabu walizopewa ikiwemo kuorodheshwa katika orodha ya mafisadi, au kusimamishwa uanachama katika vyama vya kitaaluma;

- Kuwepo kwa ujuzi na utaalam katika vyombo vya udhibiti ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa wahasibu, wakaguzi wa mahesabu, wanasheria, na waandishi wa habari waliobobea katika mambo ya fedha na habari za uchunguzi;

(iv) Toa ripoti za zamani zilizokwishaandikwa juu ya tathmini ya uadilifu wa makampuni nchini, ikiwa ni pamoja na tathmini ya kuwepo kwa rushwa katika sekta hiyo.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

LENGO LA NNE: Kuhakikisha kuwa makampuni yanawatendea haki wadau, wakiwemo wanahisa, waajiriwa, wanajamii na wazabuni

SWALI LA 1: Ni kwa kiasi gani mfumo mzima wa utawala wa kikampuni unalinda haki za wanahisa?

VIASHIRIA

(i) Tayarisha jedwali linaloonyesha haki na wajibu wa wanahisa wa aina zote wakiwamo wale wasiopiga kura na wale wenye asilimia ndogo ya hisa na kisha onyesha sheria zinazolinda haki hizo;

(ii) Eleza kwa kina ni mbinu, asasi, sera na taratibu zipi zilizowekwa kuhakikisha kuwa wanahisa wa madaraja mbalimbali wanapewa haki zao na kutendewa mambo kwa usawa;

(iii)Eleza kwa kina ni kwa namna gani wanahisa wanaweza kufidiwa endapo watakuwa wamenyimwa haki zao na ni kwa kiwango gani cha ufanisi hayo yanafanyika.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Je mfumo mzima wa Utawala wa Makampuni unatambua haki za wadau (zaidi ya wanahisa)?

VIASHIRIA

(i) Eleza kwa kina sheria, maadili ya kujiwekea wenyewe na sera zinazoongoza mahusiano ya moja kwa moja kati ya makampuni na wadau mbalimbali k.m. sheria ya walaji, sheria za kazi, haki za wakopeshaji, sheria ya mufilisi n.k.

(ii) Tathmini ufanisi wa yale uliyoorodhesha hapo juu hasa kuhusiana na:

- Uwezo wa wadau kupata habari wanazohitaji juu ya makampuni na aina ya habari zinazopatikana;

- Kiasi cha uwakilishi na ushiriki wa wadau katika kamati za makampuni na hatua za kuhakikisha kuwa bodi za wakurugenzi zinazingatia maslahi ya wadau (k.m wafanyakazi, wakopeshaji, walaji, wazabuni, na jamii iliyowazunguka) katika kufanya maamuzi;

.

(iii)Eleza ni kwa namna gani wadau wanaweza kudai fidia endapo watanyimwa haki zao.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika, ukitofautisha baina ya wadau wa aina mbalimbali kama waajiriwa, wakopeshaji, vikundi vya mazingira, n. k.

LENGO LA TANO: Kuhakikisha kuna kuwajibika kwa makampuni, wakurugenzi na maafisa

SWALI LA 1: Je mfumo mzima wa utawala wa makampuni unawezesha makampuni kutoa habari sahihi na kwa wakati kuhusu makampuni yenyewe?

VIASHIRIA

(i)Tayarisha jedwali la shuruti kuhusu utoaji habari za mambo ya kifedha na yasiyo ya kifedha kwa makampuni ya sekta ya umma na binafsi na mbinu zitumiwazo kutathmini, kusimamia, kuangalia na kuyafanya makampuni yatii shuruti hizo;

(ii)Tathmini ufanisi wa vyombo vya usimamizi katika kuangalia, utiifu wa makampuni katika kufuata shuruti za utoaji wa habari;

(iii)Elezea adhabu zinazotolewa kwa makampuni yasiyotii shuruti (k.m. onyo, faini, kusitishwa kwa uanachama, karipio, adhabu ya kimadai, adhabu ya kijinai n.k.) na ushahidi wa utekelezaji wa suala hilo kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita.

(iv) Eleza changamoto zilizojitokeza na na namna zilivyokabiliwa

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Ni kwa kiasi gani viwango vya uhasibu na ukaguzi wa mahesabu nchini vinafanana na vile vinavyokubalika kimataifa?

VIASHIRIA

(i) Eleza viwango vya uhasibu na ukaguzi wa mahesabu vilivyopo nchini, na ikiwezekana uonyeshe kama kuna tofauti za msingi kati yake na vile vya kimataifa;

(ii) Eleza kwa kina shuruti zinazohusiana na ukaguzi wa mahesabu ya makampuni kila mwaka, ukionyesha tofauti zilizopo kati ya makampuni binafsi na yale ya umma;

(iii) Jadili taratibu na sifa zinazotakiwa kwa wale wanaotaka kuwa wakaguzi wa hesabu, na ni vyombo gani vinasimamia eneo hilo la kitaalamu na masuala ya nidhamu; ikiwa ni pamoja na suala la wakaguzi kuwajibika kueleza kwa vyombo vya usimamizi au wanahisa kuhusu kujihusisha kwa wakurugenzi na maofisa wakuu wa kampuni katika vitendo visivyo halali, ulaghai na kutoa siri za biashara.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapohitajika.

SWALI LA 3: Je mfumo wa utawala katika makampuni unaruhusu uongozi mkakati wa kampuni, bodi ya wakurugenzi kuwasimamia watendaji wa kampuni kwa karibu, na uwajibikaji wa bodi ya wakurugenzi kwa kampuni na wanahisa?

VIASHIRIA

(i) Eleza ni muundo gani unaotumika sana katika kuunda bodi za wakurugenzi, au vyombo vinginevyo vya kusimamia makampuni yaliyoandikishwa katika soko la hisa, makampuni ya serikali, makampuni madogo na ya kati (kama sheria inayataka haya ya mwisho kuwa na bodi za wakurugenzi) n.k;

(ii)Elezea mchakato wa uteuzi na uchaguzi wa wakurugenzi, vigezo vinavyoangaliwa, muundo, mafao wapatayo na majukumu muhimu ya bodi;

(iii)Elezea mchakato au taratibu zinazotumika kuhakikisha kuwa bodi inasimamia utekelazaji wa sheria zinazohusika (k.m. sheria za kodi, ushindani, kazi, mazingira, fursa sawa, na afya na usalama kazini) ikiwemo mikutano, michakato ya kufanya maamuzi, masharti ya kuhudhuria vikao, sera za maadili na jinsi ya kuamua mambo yanayohusiana na migongano ya kimaslahi;

(iv) Toa tathmini ya jumla kuhusu ufanisi wa bodi katika kutoa mwelekeo mkakati, kusimamia na kuwajibika kwa wanahisa wa kampuni;

(v) Elezea programu zilizopo za kufundisha au kuongeza ujuzi wa wakurugenzi na ni kwa kiasi gani hayo yanatumika kama kigezo cha kuchagua mtu kuwa mwana bodi.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa ushahidi pale unapoonekana kuhitajika

SEHEMU YA NNE

MAENDELEO YA KIJAMII NA KIUCHUMI

Fasili

Kwa mujibu wa Azimio la NEPAD, maendeleo ya kjamii na kiuchumi yana maana ya kuendelea kuboreka kwa ustawi wa jamii na kuinua kiwango cha maisha cha wananchi.

Sehemu hii ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi inakusudia kuonyesha juhudi na mafanikio yaliyopatikana katika kuunda sera makini na taratibu za utoaji huduma katika maeneo muhimu ya maendeleo.

Maswali ya sehemu hii yatalenga juhudi zinazofanywa na wadau wote nchini kufikia malemgo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika maeneo yafuatayo:

- Kuhimiza kujitegemea na kuongeza uwezo wa kuleta maendeleo yanayojihimili yenyewe;
- Kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ili kuwe na meendeleo endelevu na kuondoa umaskini
- Kuimarisha sera, utoaji wa huduma na kuleta matunda katika sekta muhimu za kijamii ikiwepo elimu kwa wote, kupigana na maradhi kama ukimwi na mengineyo;
- Kuhakikisha watu wanapata nishati, maji na huduma za kifedha (ikiwamo mikopo midogo midogo) masoko, na teknohama kwa bei inayofaa kwa wananchi wote na hasa kwa maskini.
- Kupiga hatua kuelekea kwenye usawa wa jinsia, na hasa katika suala la fursa sawa kwa wasichana kupata elimu katika ngazi zote
- Kuhimiza ushiriki mpana wa watu wote katika shughuli za maendeleo katika ngazi zote.

1. UTANGULIZI

Malengo sita ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi yaliyoko katika Azimio la NEPAD yanashughulikia zaidi suala la kujitegemea katika maendeleo na kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ili kuondoa umaskini. Hii ni pamoja na kuwa na sera na taratibu

za utoaji huduma katika sekta muhimu, na kuhakikisha kuwa watu wanapata huduma za jamii nzuri na wanazomudu, pamoja na kufikia usawa wa jinsia na ushiriki katika masuala ya maendeleo kwa wadau wote .

Suala la kujitegemea katika maendeleo ni suala la watu husika kumiliki na kuwa na uongozi katika mchakato wa maendeleo, kuwa na ushiriki mpana na wa kina katika masuala ya mipango ya maendeleo na papo hapo kuhakikisha kuwa mchakato wa maendeleo umejikita katika rasilimali za nchi na uwezo wa watu wake. Kumiliki na kuongoza mchakato wa maendeleo ni pamoja na mambo kama kuamua vipaumbele vya maendeleo yenyewe, kuamua rasilimali zinatakiwa zitoke wapi na uwekezaji wa watu binafsi ufanywe na watu gani na kutoka wapi.

Suala la kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ni muhimu katika kuondoa umaskini. Wakati mwingine, mchakato wa kuondoa umaskini hulazimisha kutoa misaada fulani kwa watu ili kupunguza mateso ya watu maskini na kuwaongezea fursa ya kupata huduma za jamii. Kwa hiyo basi kuna umuhimu wa kujua ni juhudi zipi zinaelekezwa ili kahakikisha kuwa maskini wanapata chakula, makazi, huduma za afya, elimu, n.k. Ina maana pia kuwa kuna haja ya kuwaongezea uwezo wao wa kujiingizia kipato ili waweze kujihudumia wenyewe katika baadhi ya mahitaji yao.

Kwa sababu hiyohiyo, kuna umuhimu pia wa kuimarisha sera, taratibu za kutoa huduma na uzalishaji katika maeneo muhimu ya maendeleo ya kijamii. Maeneo ambayo yanahitaji kipaumbele ni elimu, afya, Ukimwi, hadhi ya watoto, usawa wa jinsia, kulinda makundi maalum, n.k. Katika miongo miwili iliyopita hudunma za jamii zilirudi nyuma kutokana na mageuzi ya kiuchumi yaliyokuwa yanaendelea. Hilo limechangia sana kurudisha nyuma mafanikio yaliyokwishapatikana katika vigezo mbalimbali vya huduma za jamii ikiwamo kushuka kwa idadi ya watoto walioandikishwa shule, kuongezeka kwa vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano, kuongezeka kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi, ajira ya watoto, kupungua kwa maeneo yanayopatiwa chanjo, na kuongezeka kwa viwango vya watotot wenye utapiamlo n.k. Kuimarika kwa viashiria vya kijamii sio tu kwamba ni lengo la kimaendeleo bali hatimaye kunasaidia kuharakisha

kasi ya maendeleo yenyewe. Kwa hiyo, kuna haja ya kubadili mwelekeo usioridhisha wa vigezo tulivyovitaja hapo juu kama tunataka kuwa na maendeleo endelevu.

Juhudi yabidi zifanywe ili kuongeza uwezo wa watu kupata maji, huduma za majitaka na taka ngumu, mikopo midogo midogo, masoko, na teknohama, hasa kwa watu wa vijijini ili kuimarisha njia za kujipatia riziki na kuondoa umaskini. Maendeleo yanahitajika pia katika suala la usawa wa jinsia na hasa suala la fursa sawa kwa wavulana na wasichana katika kupata elimu katika ngazi zote. Kuhimiza usawa wa jinsia kunahitaji mabadiliko katika baadhi ya sheria na mila, na kuondoa vikwazo ambavyo vinavyopelekea kuwapo kwa tofauti zilizopo. Umiliki wa ardhi, kwenda shule na ajira ni baadhi ya maeneo ambapo kukosekana kwa usawa wa jinsia kumekithiri.

Ili kufikia malengo ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, ushiriki mpana na wa kina wa wadau wote katika ngazi zote ni muhimu.

Kwa kila moja kati ya malengo haya, kuna maswali yanaulizwa na viashiria vitakavyoibua matatizo ya kimfumo yaliyo katika jamii na jinsi yanavyoathiri masuala ya maendeleo vimetolewa kuhusiana na jinsia, kiasi, ushirikishaji, na uendelevu. Maswali hayo na viashiria hivyo vinakusudiwa kutoa majibu yatakayosaidia kupima maendeleo kwenye sekta muhimu za maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Tafadhali jibu kila swali na viashiria vilivyotajwa. Viashiria vya ziada ambavyo vinaonekana muafaka vinaweza kutumika. Tafadhali andika chanzo ambacho kinaweza kuthibitisha majibu yako. Kwa upande wa vigezo vya uwingi, tafadhali andika thamani ya kitakwimu ya kila kigezo. Kwa upande wa vigezo vya ubora, tafadhali toa maelezo mafupi lakini yaliyo fasaha. Katika vigezo vyote viwili, toa maelezo ambayo yanaonekana kuwa ya muhimu na rejea ya chanzo cha takwimu

Tafadhali jibu swali la kwanza kwakila kiwango na maadili yaliyoorodheshwa. Tafadahali jisikie uko huru kuongeza viwango na maadili ambayo hayakujumuishwa katika orodha hii

2. VIWANGO NA MAADILI

- Waraka wa Mpango-sheria wa NEPAD
- Haki ya Maendeleo iliyopo katika Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Watu (1981) ikiwa ni pamoja na itifaki kuhusu Haki ya Wanawake wa Afrika
- Mkataba wa Afrika wa Ushirikishaji Wananchi katika Maendeleo (1990)
- Mkutano wa Dunia kuhusu Maendeleo Endelevu (WSSD) Johannesburg (2002)
- Azimio la Karne la Umoja wa Mataifa (2000)
- Azimio la Umoja wa Matiafa kuhusu Haki ya Maendeleo
- Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto (1990)
- Mkutano wa Dunia kuhusu Mpango wa Utekelezaji wa Maendeleo ya Kijamii (1995)
- Sheria ya Awali ya Kuunda Umoja wa Afrika
- Mkataba kuhusu Uondoaji wa Aina zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (Jukwaa la Utekelezaji Mipango Beijing)

3. SWALI LINALOHUSIANA NA VIWANGO NA MAADILI

SWALI: Ni kwa kiasi gani nchi yako imechukua hatua za kusaini, kuridhia, kutumia na kufuata kikamilifu viwango hivi?

VIASHIRIA

(i) Onyesha ushahidi wa kutia saini, kuridhia, au kukubali kila kiwango kimoja kimoja;

(ii) Hatua gani zinachukuliwa kuridhia au kufuata viwango hivi?

(iii) Kama nchi yako haijaridhia viwango na maadili hayo hapo juu, kuna sheria, sera, au miongozo ipi mingine inayotumika?

(iv) Onyesha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kusahihisha mapungufu na matatizo ya uwezo mdogo;

(v) Elezea maendeleo yaliyopatikana katika kufikia viwango au malengo kwa kutumia vipimo muafaka.

4. TATHMINI ZILIZOPITA

4. 1 Tafadhali toa nakala za tathmini ambazo nchi yako ilishawahi kufanya katika suala la **Maendelo ya Kijamii na Kiuchumi** ambazo zitasaidia nchi yako kujitathmini;

4. 2 tafadhali toa nakala za tafiti nyingine zilizowahi kufanyika katika eneo hilo la **Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi** ambazo unadhani zinaweza kusaidia katika kutathmini nchi yako.

5. MASWALI YANAYOHUSU MALENGO

LENGO LA KWANZA: Kuhimiza kujitegemea na kuongeza uwezo kwa ajili ya maendeleo yanayojihimili yenyewe

SWALI LA 1: Ni kwa kiasi gani nchi inamiliki mchakato na usanifu wa mipango ya

ya taifa maendeleo?

VIASHIRIA

(i) Eleza hatua zinazofuatwa katika kusanifu na kutekeleza mipango ya taifa ya maendeleo, na utaje wadau wote wanaoshiriki katika mchakato mzima;

(ii) Tathmini namna miradi ya maendeleo inavyokidhi mahitaji halisi ya watu;

(iii) Elezea ni njia gani zinatumika kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kumiliki mipango na programu za maendeleo, ikiwemo mafunzo, kufuatilia na tathmini.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Je fedha za kuendesha mpango wa maendeleo wa taifa zinatoka wapi?

VIASHIRIA

(i) Toa asilimia za rasilimali toka nje na zile za ndani zinazotumika kuendesha bajeti ya taifa, hasa mipango ya taifa ya uwekezaji;

(ii) Tathmini kiasi cha utegemezi wa nchi kwa misaada ya nje kuhusiana na:

- Deni la taifa kama sehemu ya pato la taifa
- Kiasi kinachotumika kulipa madeni kama sehemu ya mauzo nje ya nchi.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

LENGO LA PILI: Kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi ili kuwe na maendeleo endelevu na kuondoa umaskini

SWALI LA 1: Je nchi yako inafanya nini kuharakisha maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupata maendeleo endelevu na kuondoa umaskini?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kuwepo kwa hatua za kisheria, kisera, na kiasasi za kuharakisha maendeleo endelevu na kuondoa maskini;

(ii) Toa maelezo ya kina kuhusu ukubwa na vigezo vinavyotumika kugawa rasilimali zinazokusudiwa kuharakisha maendeleo endelevu na kuondoa umaskini;

(iii) Eleza changamoto zilizopatikana kwenye mchakato huo na jinsi gani zilikabiliwa na hatua gani zimechukuliwa kulinda mafanikio yaliyopatikana;

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Ni yapi matokeo ya sera na michakato ya kuleta maendeleo endelevu na kuondoa umaskini?

VIASHIRIA

(i)Elezea matokeo yaliyopatikana kwa kuangalia:

- Kukua kwa pato la taifa, ikiwa ni pamoja na kukua kwa pato la taifa kwa kila raia katika miaka mitano iliyopita,
- Vigezo vya malengo ya milenia,
- Vigezo vya WSSD,
- Vigezo vya maendeleo ya jamii kwa kuvigawa katika makundi ya jinsia, hali ya vijijini, hali ya mijini

(ii) Elezea hatua zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto zilizopatikana kwenye mchakato huo ikiwamo namna ya kusimamia na kutathmini mafanikio yaliyopatikana;

Vigezo vya ziada vyaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira maalum na uzooefu uliopo nchini

LENGO LA TATU: Kuimarisha sera, utoaji wa huduma na matokeo katika sekta muhimu za kijamii ikiwepo elimu kwa wote, kupigana na maradhi kama ukimwi na maradhi mengineyo ya kuambukiza.

SWALI LA 1: Serikali imechukua hatua gani kuimarisha sera, taratibu za utoaji huduma, na suala la kufuatilia matokeo ili kufikia malengo ya maendeleo ya kijamii?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kuwepo kwa hatua za kisheria, kisera, na kiasasi za kuimarisha utengenezaji wa sera na taratibu za utoaji huduma;

(ii) Toa maelezo ya kina kuhusu ukubwa na vigezo vya mgawanyo wa rasilimali zinazokusudiwa kutumika kufikia malengo ya maendeleo ya kijamii;

(iii)Toa ushahidi wa ushiriki wa wadau wote katika kutengeneza sera, taratibu za utoaji huduma na ufuatiliaji wa matokeo;

(iv) Onyesha changamoto zilizojitokeza na juhudi za kushughulikia vikwazo vilivyojitokeza.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

SWALI LA 2: Je sera na michakato vimekuwa na athari gani kwenye vigezo vya kijamii?

VIASHIRIA

Elezea mwelekeo wa vigezo vya maendeleo ya jamii katika miaka 5–10 iliyopita kwa kuangalia yafuatayo;

(i) Afya, na hasa vifo vya watoto na malaria;

(ii) Kiwango cha kuenea kwa virusi vya ukimwi na maradhi mengine ya kuambukiza; onyesha kiwango kwa kufuata misingi ya jinsia, na tofauti baina ya vijijini na mijini;

(iii) Elimu, hasa kwa kuangalia uandikishaji wa wasichana shuleni ikiwa ni pamoja na vyuo vya elimu ya juu na vyuo vinginevyo;

Vigezo vya ziada vyaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira maalum na uzooefu uliopo nchini

LENGO LA NNE: Kuhakikisha watu wanapata nishati, maji, huduma za maji taka na taka ngumu, huduma za kifedha (ikiwamo mikopo midogo midogo), masoko, teknohama, makazi na ardhi kwa bei inayofaa na hasa kwa maskini wa vijijini

SWALI LA 1: Je, serikali imeweka sera gani ambazo zinahakikisha kuwa wananchi wote, na hasa wale maskini wa vijijini na mijni wanapata huduma muhimu na wanazomudu?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kuwepo kwa hatua za kisheria, kisera, na kiasasi za kahakikisha kuwa watu wanapata huduma muhimu kwa bei watakayomudu;

(ii) Toa ushahidi kuhusu ukubwa na vigezo vinavyotumika kugawa rasilimali hizo;

(iii) Eleza mafanikio yaliyopatikana kwa kuangalia:

- Asilimia ya wananchi kwa mikoa, makazi, jinsia, matabaka katika jamii n. k. wenye kupata huduma muhimu za kijamii kwa bei nafuu;

- Upatikanaji na ufikishaji wa huduma muhimu kwa watu maskini wa vijijini, mijini na makundi mengine maalum;

- Athari zitokanazo na ubinafsishaji wa huduma muhimu kama zipo

(iv) Onyesha changamoto zilizojitokeza na namna vikwazo hivyo vilivyoshughulikiwa;

Vigezo vya ziada vyaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira maalum na uzooefu uliopo nchini

LENGO LA TANO: Kupiga hatua kuelekea kwenye usawa wa jinsia katika maeneo yote muhimu, hususan fursa sawa kwa wasichana kupata elimu katika ngazi zote

SWALI LA 1: Je nchi imechukua hatua gani kuingiza suala la jinsia katika mipango yake na kumekuwa na mafanikio kiasi gani?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kuwepo kwa hatua za kisheria, kisera, na kiasasi za kuhamasisha usawa wa jinsia;

(ii) Toa ushahidi wa kuwepo kwa malengo maalum katika kufikia usawa wa jinsia katika maeneo muhimu;

(iii) Toa maelezo ya kina kuonyesha kuwa rasilimali zimeelekezwa kwenye usawa wa jinsia na hasa katika bajeti ya serikali;

(iv) Toa ushahidi ya mafanikio yaliyopatikana hususan kuhusu mwelekeo wa:

- Ushiriki na uchangiaji wa wanawake katika masuala muhimu ya kiuchumi na kijamii,

- Takwimu za jinsia katika elimu katika ngazi zote,

- Ushiriki wa wanawake katika nafasi za kufanya maamuzi,

- Viashiria vinginenevyo vinavyoonyesha tofauti za kijinsia (kwa mfano tofauti ya mapato na mishahara),

(v) Toa maelezo ya kina kuhusu ripoti zilizotangulia au tathmini juu ya hali ya jinsia hapa nchini.

Tafadhali toa maelezo ya kina huku ukitoa uhahidi pale unapohitajika

LENGO LA SITA: Kuhimiza ushiriki mpana wa wadau wote katika shughuli za maendeleo katika ngazi zote

SWALI LA 1: Taratibu gani zimewekwa kuhimiza ushiriki wenye ufanisi wa wadau muhimu katika mchakato mzima wa maendeleo?

VIASHIRIA

(i) Toa ushahidi wa kuwepo hatua za kisheria, kisera na kiasasi kuhakikisha kuwa wadau wote kwa mapana yake wanashiriki katika mchakato mzima wa maendeleo wakiwamo wanajamii, sekta binafsi, vyombo vya habari, jumuia za vijijini, vikundi vya wanawake, makundi maalum n.k.;

(ii) Eleza namna ulivyo mfumo wa utawala, na hasa kuhusiana na kubajeti na mchakato wa kutoa fedha za bajeti;

(iii) Tathmini ufanisi wa hatua zilzochukuliwa kuhakikisha kuna ushiriki mpana katika mambo ya maendeleo

(iv) Onyesha changamoto zilizojitokeza na hatua zilizochukuliwa kulinda mafanikio yaliyopatikana (ikiwa ni pamoja na mafunzo, usimamizi, tathmini na urekebishaji wa hali).

Vigezo vya ziada vyaweza kuongezwa ili kuakisi mazingira maalum na uzooefu uliopo nchini